SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Lipumba** aibuka na Katiba 'viraka'

UKURASA 3



DE JONG KUTIMKA BARCELONA

UKURASA 22

Nipashe
Jumatatu Desemba 27, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579807
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Waziri wa Afya ajitangaza kupata UVIKO-19

UKURASA 5



Waumini wa Kanisa Katoliki Mtinko, Parokia ya Mtakatifu Karolas, Halmashauri ya Wilaya ya Singida walijitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 baada ya kumalizika kwa ibada ya Jumapili ya Sikukuu ya Krismasi, jana. **PICHA: MARY GODFREY**

## YALIYOMO

UKURASA WA 17

**WANNE WAFARIKI KWA KULA SAMAKI MWENYE SUMU**

WATU wanne wamefariki dunia na wengine zaidi ya 30...

## Matatani tuhuma za kuua mama mzazi, mwili wakutwa chemba ya choo

UKURASA 2



Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Juma Kimori (katikati), Meneja Mwandamizi Idara ya Biashara za Kadi, Manfred Kayala (kushoto) na Mchambuzi wa masuala ya Kadi na Fedha, Helga Loth, wakizindua rasmi kampeni ya 'MastaBata Kivyako Vyako' jijini Dar es Salaam juzi. Benki ya NMB imezindua msimu wa tatu wa promosheni ya matumizi ya kadi, zaidi ya Sh. milioni 240 zitazawadiwa kwa washindi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Aliyetangazwa 'kufariki' azinduka

UKURASA 2

MICHEZO CITY YASALIMU AMRI KWA SIMBA, YANGA UK.20 | MAONI, KATUNI UK.6



Baba mzazi wa Ayuba Mawazo (26), Mwazo Awadi, akiwa amempakata mwanawe Ayuba ambaye alidhaniwa kufariki na baadaye kuzinduka ghafla hali iliyoleta taharuki kwa wananchi wa Masasi, jana. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Aliyetangazwa 'kufariki' azinduka

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

MKAZI wa Kijiji cha Msikisi wilayani Masasi, mkoani Mtwara, Ayuba Mawazo (26), aliyedaiwa kufariki dunia, na wananchi kufika nyumbani kwa shughuli za mazishi, amezinduka na kuomba apewe uji.

Awali, familia yake ilitangaza msiba wa kijana huyo na kusababisha wananchi kukusanyika nyumbani kwao kuendelea na shughuli za msiba, lakini baadaye familia hiyo ilitangaza kuwa mgonjwa wao alikuwa amepoteza fahamu wakati akiwa mahututi.

Hali hiyo ililazimu familia kuwaeleza wananchi waliokusanyika nyumbani hapo kuwa hakuna msiba.

Kutokana na taarifa hizo wananchi wa kitongoji hicho iliwabidi waanze kutawanyika na kurudi makwao.

Akizungumza na Nipashe jana kijijini hapo, baba mzazi wa kijana huyo, Mawazo Awadi, alisema mtoto wao ni mgonjwa na walimpeleka Hospitali ya Mkomaindo Halmashauri ya Mji wa Masasi Desemba 21, mwaka huu, kwa matibabu na baadaye walimtoa, lakini wakiwa njiani alipoteza fahamu na kudhani kuwa amefariki dunia.

"Ni kweli kijana wetu anaumwa na tulimtoa hospitali akiwa mzima ila hali yake ilikuwa mbaya na tulipofika nyumbani tulikuta wananchi wamekusanyika na mgonjwa tulipomwingiza ndani alizinduka ghafla na kuomba uji, hali inayoonyesha alikuwa amepoteza fahamu tu si kifo," alisema Awadi.

Alisema walipofika hospitali kijana wao alilazwa kutokana hali yake kuwa mbaya na kusababisha kupoteza fahamu hali iliyowatia wasiwasi wanafamilia.

Awadi, alisema Desemba 23, majira ya alasiri hali ya mgonjwa ilikuwa mbaya zaidi kiasi cha kushindwa kutambua wanaongia wodini kumwangalia na kushindwa kula chakula na kusababisha wanafamilia kuomba kuruhusiwa kurudi nyumbani na mgonjwa wao.

Alisema uongozi wa Hospitali ya Mkoamaindo ulikataa kuwapa ruhusa kwa sababu hali ya mgonjwa ilikuwa mbaya.

Hata hivyo, wanafamilia walishurutisha kuondoka na mgonjwa wao na uongozi wa hospitali uliamua kutoa masharti ya kujaza fomu maalumu ya kujieleza kwanini waondoke na mgonjwa ilhali yupo na hali mbaya na walifanya hivyo na kuondoka kurudi kijijini.

Alisema wakati wanarudi nyumbani baadhi ya wanafamilia waliokuwa ndani ya gari la mgonjwa huyo aliyekuwa amepoteza fahamu walihisi ameshafariki na kutoa taarifa kijijini kuwatangazia wananchi kushiriki shughuli za msiba.

Alieleza kuwa waliingia ndani na mgonjwa huyo na ghafla alipiga chafya na kuzinduka na kuomba apewe uji anywe.

Wakizungumza na gazeti hili nyumbani kwa mgonjwa huyo, baadhi ya wananchi walisema walipewa taarifa na mmoja wa familia kuwa mgonjwa amefariki na wapo njiani kurudi kijijini wakiwa na maiti kwenye gari.

Danford Kiliani, mkazi wa kijiji hicho alisema baada ya kupata taarifa ya kifo cha mwanakijiji mwenzao, walifika nyumbani kwa familia hiyo na kupokea mwili wa kijana huyo, lakini muda mfupi baadaye wananchi walijulishwa kuwa maiti amezinduka na sasa anaomba kupatiwa uji anywe.

Naye Fidea Luka mkazi wa Kijiji cha Msikisi, alisema anashangazwa na baba mzazi wa kijana huyo kuwatupia lawama wanakijiji kuwa walisambaza taarifa za ndugu yao kufariki na baadaye kuzinduka wakati ukweli ni kwamba familia yenyewe inahusika na mkanganyiko huo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Msikisi, Emmanuel Mrope, alisema taarifa ya awali iliyotolewa na wanafamilia wa kijana huyo ilisema wazi kuwa mgonjwa amefariki na kuwaomba wanakijiji waende sehemu husika kwa ajili ya shughuli za taratibu za mazishi.

Alisema baadaye familia hiyo iligeuka na kutoa taarifa mpya ikieleza kuwa kijana wao waliyedai amefariki amezinduka na ameomba uji.

Kadhalika alisema familia hiyo ilisema ndugu yao hajapoteza maisha bali alikuwa amepoteza fahamu na kuwatangazia wananchi waliokuwa wamekusanyika sehemu ya tukio wakaendelee na shughuli zao kama kawaida.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, Kaimu Mganga Mkuu wa hospitali hiyo, Grace Mnengena, alisema walimpokea mgonjwa Desemba 21 na kutoka na hali aliyokuwa nayo walimlaza wodi namba moja na baada ya vipimo alikugundulika kusumbuliwa na tatizo la sukari kushuka.

"Familia waliondoka na mgonjwa wao hospitalini hapa akiwa bado mzima ila hali yake ilikuwa mbaya kiasi cha kupoteza fahamu mara kwa mara na wanafamilia walipoomba kuondoka na mgonjwa wao bila ya ruhusa ya daktari walikubali kujaza fomu ya maelezo maalumu," alisema Mnengena.

Alisema wakati wanafamilia wanaondoka hospitali na mgonjwa wao, alikuwa katika hali mbaya ya kutojitambua na walisisitiza kwenda kwenye tiba asili kwa vile hawana fedha za kuendelea kukaa naye hospitali.

## Matatani tuhuma kuua mama mzazi, mwili wakutwa chemba ya choo

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

MKAZI wa Njiro Kontenda Kata ya Engutoto jijini Arusha, Patrick Mmasi (24), anashikiliwa na Polisi kwa tuhuma za kumuua mama yake mzazi, Ruth Mmasi (40) na kuutumbukiza mwili wake kwenye chemba ya choo ya majitaka.

Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, Justine Masejo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kumshikilia Mmasi kwa tuhuma za kifo cha utata cha mama yake.

Alisema walimshikilia kijana huyo kwa ajili ya uchunguzi zaidi na upelelezi utakapokamilika atafikishwa mahakamani.

Kwa mujibu wa ndugu wa marehemu, Ruth atazikwa kesho alasiri Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara.

Aidha, ndugu wa marehemu ambaye hakutaja jina lake, alisema kuwa tukio hilo liligundulika Desemba 24, mwaka huu, baada ya polisi kufika nyumbani kwa marehemu kufanya upekuzi na kubaini mwili ukiwa ndani ya chemba ya choo.

Kwa mujibu wa ndugu huyo, mtoto mwingine wa marehemu, Patricia Mmasi (19), anayesoma nchini China, alipata shaka akiwa nchini humo baada ya kumtafuta mama yake kwenye simu bila mafanikio.

Alisema aliamua kusafiri kurudi nchini Tanzania kwa sherehe za Krismasi na kumuuliza kakaye Patrick kuhusu kutoonekana na kutopatikana kwenye simu mama yao, na baada ya kutopata majibu ya kuridhisha yeye na ndugu wengine waliamua kutoa taarifa polisi.

Aliongeza kuwa polisi walipofika walifanya upekuzi katika sehemu mbalimbali za nyumba hiyo ya ghorofa moja, walibaini mwili huo ukiwa ndani ya chemba ya choo nyuma ya nyumba hiyo.



Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuiomba serikali kufanya mabadiliko madogo ya Katiba. Kulia ni Naibu Mkurugenzi wa Mambo ya Nje wa chama hicho, Jafari Mneke. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Lipumba aibuka na Katiba ya viraka

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahimu Lipumba, amependekeza wadau wa siasa kutumia fursa waliyopewa na Rais Samia Suluhu Hassan, kukaa pamoja na kupeleka mapendekezo ya kuishauri serikali ifanyie marekebisho madogo ya Katiba ya sasa kwa kuweka viraka ili iwe rahisi kupata Tume Huru ya Uchaguzi itakayosimamia uchaguzi wa 2024 na 2025.

Prof. Lipumba alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema hivi karibuni katika kongamano la kujadili maendeleo ya demokrasia nchini, Rais Samia katika hotuba yake alisema yuko tayari kusikiliza, kupokea na kufanyia kazi mapendekezo yatakayopelekwa na wadau wa vyama hivyo na kwamba ni vyema kutumia fursa hiyo kujadili suala hilo.

Prof. Lipumba alisema miongoni mwa vitu vilivyojadiliwa na kuridhiwa na wadau walioshiriki katika kongamano hilo la Dodoma la demokrasia ni pamoja na kupata Katiba mpya na kwamba kwa kuwa mchakato wa kupata Katiba hiyo mpya unaweza kuchukua muda mrefu ni vyema wakubaliane kufanyia marekebisho madogo Katiba ya sasa na baadaye ikipatikana tume huru wataendelea na mchakato wa kuikamilisha.

"Kwa mujibu wa sheria, tume huru ya uchaguzi inapaswa iwe imeteuliwa miaka mitatu kabla ya uchaguzi, na sisi tunataka uchaguzi ujao wa serikali za mitaa na ule mkuu zote zisimamiwe na tume iliyo huru, kwa hiyo ni vyema tukatumia fursa hii kushirikiana kupeleka mapendekezo kwa Rais ya kufanyia marekebisho madogo ya Katiba ili kufikia mwakani yawe yamekamilika," alisema Prof. Lipumba.

"Na kwa nini tunahitaji mabadiliko madogo ya Katiba yafanyike mapema, ni kuwezesha kuandaa uchaguzi ulio huru na wa haki mwaka 2024 na 2025. Kwa hiyo nilikuwa nataka tutumie nafasi kupitia kauli ya Rais kwamba yuko tayari kupokea mapendekezo, tusisitize kwamba mchakato wa mabadiliko ya madogo ya Katiba yafanyike mwaka 2022."

"Sheria ya uchaguzi itungwe upya kwa kuzingatia kuwapo kwa tume huru ya uchaguzi na wajumbe wa tume wenye sifa waombe na wateuliwe ili ianze kazi mapema kuandaa uchaguzi ujao. Lakini kwa sababu ya kadhia zinazojitokeza katika uchaguzi wa serikali za mitaa, ni bora tume hiyo huru itakayoundwa ya uchaguzi ikasimamia chaguzi zote, kuanzia wa serikali za mitaa, uchaguzi wa diwani, mbunge na rais."

Prof. Lipumba alisema endapo watasema kwa sasa waanze na Rasimu ya Jaji Joseph Warioba ambayo ilitoa msimamo wa mfumo wa muungano wa serikali tatu au ile inayopendekezwa yenye muungano wa serikali mbili, lazima kufanyike maridhiano ya muafaka wa kitaifa ya ipi itumike.

"Lakini tusisubiri kulikamilisha hili kwa sababu tuna uhitaji wa haraka wa tume huru ya uchaguzi ambayo karibu wadau wote wameridhia kwamba kwa kweli inahitajika. Na tunaamini kwamba tukimaliza hili, tutakamilisha na hilo la Katiba Mpya, niombe wadau wote tutumie fursa hii tushirikiane kulisukuma hili la marekebisho madogo ya Katiba ya sasa."

Kwa mujibu wa Prof. Lipumba, endapo Rais Samia atatekeleza yale aliyoahidi katika mkutano wa wadau hao wa demokrasia atakuwa amejijengea historia kubwa.

"Kwa hiyo, nampongeza Rais Samia kwa hotuba aliyoitoa katika kongamano la demokrasia, lakini natoa wito kwa sisi wanasiasa, tulitazame hili kama fursa ya ukosefu wa demokrasia, panapopatikana fursa ya kupata maridhiano na kulisukuma hili gurudumu la kupata mfumo mzuri wa demokrasia, fursa hiyo tusiipoteze, tuitumie," alisema Prof. Lipumba.

"Tulikubaliana kwamba tupate Katiba Mpya kwa kuanzia pale tulipoishia, lakini ikasemekana kwamba mchakato unaweza kuchukua muda mrefu, tunahitaji kuwa na uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024, sasa ili kunusuru haya, hili la kufanya marekebisho madogo inakuwa ni mchakato wa mpito kuelekea katiba mpya, kwamba tunaiwekea kiraka hii ya sasa kusudi tuhakikishe unapata tume huru ya uchaguzi, halafu tunaendelea. Sasa ikiwa tutasubiri tunaweza kujifunga goli wenyewe na hatutakuwa na muda wa kutosha wa kupata tume huru ya kusimamia uchaguzi ujao."

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA UJENZI WA HUDUMA ZA UGAVI WA MAJI KWA MRADI WA EACOP KUMBUKUMBU NA. ECP-21-C-015**

KAMPUNI ya Mafuta na Gesi ya TOTAL East Africa Midstream BV (Company) Tanzania, inawaalika wakandarasi wazoefu na wanaoheshimika ambao wana uwezo unaoonekana, uzoefu uliothibitishwa, utayari na uwezo wa kueleza nia yao ya kutoa huduma zifuatazo kwa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. mradi wa EACOP.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Ujenzi wa mifumo ya maji chini ya ardhi / visima kama ifuatavyo:

1.Uchimbaji wa Visima vya Majaribio kabla ya uendelezaji kamili wa visima kwa madhumuni ya uzalishaji

2.Shughuli za Kuchimba visima

- Kuchimba visima vyema kwa kutumia Mashine ya aina ya rotary.
- Rig na njia ya kuchimba visima iliyopitishwa lazima iwe ya kufaa kwa kuchimba visima kupitia nyenzo zisizounganishwa, na mwamba mgumu, uliounganishwa.

3.Ujenzi wa Kisima ni pamoja na lakini sio zaidi ya:

- Ununuzi wa vifaa muhimu: Pampu, casings, mabomba, paneli za jua, tanki la kuhifadhi maji,…
- Ufungaji na uunganisho wa casings na skrini
- Zana na nyenzo zote muhimu kwa ajili ya kufanya shughuli za uvuvi inapohitajika
- Ufungaji wa muhuri wa saruji na pakiti ya Gravel
- Kuua vijidudu na kusafisha kisima
- Vifaa vya Juu ya ardhini (makazi, uzio n.k.)
- Vipimo vyote muhimu: Vipimo vya kusukuma maji, vipimo vya sampuli za maji na udongo, …
- Shughuli zote zitazingatia kanuni za mazingira za Tanzania,
- Shughuli, Rekodi za Kukamilisha na Ripoti

Kazi hiyo itafanywa katika maeneo mbalimbali nchini kote

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa kusajiliwa na Brela ORS, CRB, OSHA na wizara ya maji kama kampuni ya kuchimba visima
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi
- Maelezo ya uzoefu wa siku za nyuma katika kutoa uendelezaji wa visima vya maji: Mashimo ya majaribio, uchimbaji wa visima, ukamilishaji wa kisima, usakinishaji juu ya ardhi,…
- Orodha ya miradi iliyotangulia: maelezo, mteja, eneo,…
- Orodha ya mifumo na vifaa inayomilikiwa, wafanyikazi wenye vigezo na uzoefu
- Maelezo ya kina ya Mitambo ya kuchimba visima : aina, uwezo, vyeti,…
- Maelezo ya mfumo wa afya usalama na mazingira: Mpango wa HSE, taratibu za HSE, rekodi za HSE, mfano wa tathmini ya hatari,..
- Maelezo ya mfumo wa ubora
- Uthibitisho wa uwezo wa kifedha kutekeleza wigo uliopendekezwa wa huduma
- Nakala ya Sera za Kupambana na Rushwa na Maadili

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **adeline.m-mari@external.totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **9:00 mchana** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **24 Januari 2022.** Kichwa cha Barua Pepe ni ECP-21-C-015/EOI

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

# Waumini wajitokeza kuchanja UVIKO-19

**Na Mary Geofrey,** SINGIDA

WAUMINI wa madhehebu mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida, wamejitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19.

Waumini hao walipata chanjo hiyo aina ya Pfizer, muda mfupi baada ya kumalizika kwa ibada katika Kanisa ya Kiinjili ya Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Imani, Kanisa Katoliki Parokia ya Yohana Mbatizaji Mtinko na Kanisa la Pentekoste FPCT Ilongero, jana wilayani Singida mkoani Singida.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia Kitengo cha Elimu kwa Umma, inatekeleza Kampeni ya Kuhamasisha Utoaji wa Chanjo ya UVIKO-19, katika Mpango Shirikishi na Harakishi Awamu ya Pili unaoendelea kutekelezwa nchini nzima.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Victorina Lodovick, akiwa katika makanisa hayo jana kwa nyakati tofauti, aliwahimiza waumini wa madhehebu hayo, katika kusherehekea Sikukuu ya Krismasi kupata chanjo ya UVIKO-19.

Alisema ni wajibu wa serikali kuhakikisha usalama wa raia wake, Wizara ya Afya inaendelea na kampeni ya nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa ili kuwafikia wananchi wanaohitaji chanjo katika mkoa wote wa Singida.

Naye Paroko Msaidizi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Yohane Mbatizaji Mtinko, Padri Raphael Madinda, alisema mapadri walishapatiwa mafunzo kuhusu tahadhari ya ugonjwa huo na chanjo ya UVIKO-19 kutoka kwa Wizara ya Afya na ndiyo sababu ya kuendelea kuelimisha waumini wao.

Aliwataka wananchi hao kutopuuza taarifa zinazotolewa na wataalamu wa afya hasa kwa kuzingatia kuwa jana ni sikukuu ya familia takatifu ya Mungu, yaani Mariam, Yoseph na Yesu ambao wamekuwa mfano wa kuigwa.

"Kama ilivyo mfano kwa familia takatifu ya Mungu, nanyi tunawasihi wanafamilia kuzilinda familia zenu kwa kujikinga na maradhi haya, lakini kupata chanjo ya UVIKO-19," alisema Padri Madinda.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mtakatifu Carolus Mtinko, Sister Susanna Mushi, aliwaeleza waumini hao kuwa, mgonjwa wa UVIKO-19 aliyezidiwa, anatakiwa kuwekewa mitungi ya gesi ambayo haipatikani kirahisi wilayani humo.

Alisema mgonjwa mmoja anatumia mtungi mmoja kwa saa nane huenda na gharama zake ni kubwa ambazo wananchi wengi hawawezi kuzimudu.

"Kwanini tufike huko, tujitokeze kuchanja, ili kuwa na uhakika wa usalama wa maisha yetu, ukichanja huwezi kuzidiwa na utaisaidia familia yako inayokutegemea," alisema Sister Susanna.

Naye Askofu wa Kanisa la Pentekoste FPCT, Wilson Lazaro, aliwaongoza waumini wake kupata chanjo ya UVIKO-19, na kusema kuwa, msimamo wa kanisa hilo ni kuchanja ili kuamua kuondokana na dhana potofu kuhusu chanjo zinazotolewa.



Mafundi wakiendelea na uwekaji wa alama ya mpaka kati ya Tanzania na Kenya katika kijiji cha Naan wilayani Ngorongoro mkoani Arusha. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# TARURA yatakiwa kusimamia sheria

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WATENDAJI wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, wametakiwa kusimamia ipasavyo sheria zinazolinda barabara na kudhibiti watu wanaopitisha magari makubwa ya mizigo, ili kuepusha barabara kuharibika haraka.

Akizungumza katika kikao cha kuwasilisha mpango wa bajeti wa matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa madiwani, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Bukoba, Murshid Ngeze, alisema barabara nyingi zinatengenezwa na kuharibika haraka kutokana na kuruhusu magari yenye uzito mkubwa.

"Makalavati yanaharibika kila mwaka kutokana na kupitisha magari ya mizigo, nenda barabara inayotoka Rubale kuelekea Nsheshe, makalavati yote yana matundu, sio kwa sababu yametengenezwa kwa muda mrefu, ni kwa sababu yanapitisha magari ya mizigo ambayo yanazidi uwezo wa barabara," alisema. Ngeze ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) taifa, alisema asilimia kubwa ya barabara hizo zimetengenezwa kupitisha magari ya abiria yanayokwenda vijijini kama hiace na madogo ya mizigo, na kwamba wanaporuhusu yenye uzito usiostahili ni uharibifu wa barabara na watakaokiuka ili kulinda barabara. Akiwasilisha taarifa hiyo, Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Bukoba, Kenneth Dushime, alisema kuwa kwa mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 wanatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 2.2 kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Akitoa mchanganuo wa bajeti hiyo, alisema zaidi ya Sh. milioni 776.4 zitatokana na fedha za mfuko wa barabara, Sh. bilioni moja kutoka fedha za tozo ya mafuta na Sh. milioni 500 kutoka fedha za Mfuko wa Jimbo.

Naye Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Fatna Laay, aliwashauri madiwani kupitia orodha ya barabara zilizopangwa kutengenezwa na TARURA katika kipindi hicho, ili kama kuna ambazo si kipaumbele watoe mapendekezo kwa wakala kwa ajili ya mabadiliko.

"Lengo la kutengeneza barabara ni kuondoa kero kwa wananchi, kwa sababu madiwani barabara zenu mnazijua na mnajua ipi muhimu zaidi ya nyingine, siyo mbaya mkitoa mapendekezo ipi ianze kutengenezwa," alisema Laay.

Baadhi ya madiwani waliohudhuria kikao hicho akiwamo Samwel Makwabe wa Kata ya Karabagaine, wameitaka TARURA kuongeza upana wa barabara za vijijini, ili kuruhusu magari kupita kwa urahisi.

# 'Mastabata-Kivyako Vyako'

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imezindua msimu wa tatu wa kampeni ya kuhamasisha matumizi ya kadi na Masterpass QR iitwayo 'NMB MastaBata - Kivyako Vyako'.

Katika kufanikisha kampeni hiyo, NMB imetenga Sh. 240 zitakazoshindaniwa katika kipindi cha wiki 10.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa promosheni hiyo jijini Dar es Salaam, Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Juma Kimori, alisema kwa kipindi hiki zawadi ni pesa taslimu ili kuwapa uhuru washindi kuzitumia wanavyotaka.

Alisema tofauti na misimu iliyopita ya 'NMB MastaBata' na 'NMB MastaBata – Sio Kikawaida,' iliyohusisha zawadi za bidhaa mbalimbali, kampeni hiyo msimu huu itatoa zawadi za pesa taslimu kwa wateja 1,080, uamuzi unaolenga kumpa mteja uhuru wa kuchagua matumizi ya pesa.

"Promosheni hiyo mpya inayojulikana kama NMB MastaBata, Kivyako Kivyako, ilianza rasmi mwisho wa wiki na itaendelea kwa muda wa wiki 10 mfululizo huku zawadi zikitolewa kila mwisho wa mwezi," alisema Kimori.

Kimori alisema tangu mwaka 2018, NMB imekuwa ikiendesha kampeni za MastaBata kuchagiza matumizi ya kadi za NMB Mastercard naMasterpass QR miongoni mwa wateja wake.

Alisema washindi wa kila wiki watanyakua Sh. 100,000 na Shilingi milioni moja kila mwezi kwenye droo ya mwisho, washindi 30 watashinda Sh. milioni 90.

"Ili kurudisha faida tunayoipata kama benki kwa wateja wetu, tumezindua promosheni hii itakayoshuhudia zawadi ya pesa taslimu zikitolewa kwa wateja wetu na pesa hii itawekwa katika akaunti zao ili kuwahamasisha waendelee kufanya malipo kwa kadi au Masterpass QR," alisema Kimori.

Alisema mbali na kuhamasisha malipo ya kidijitali na kusaidia juhudi za kuifanya Tanzania kuwa uchumi usiotegemea sana pesa taslimu, pia NMB inaitumia kampeni hiyo kuwalipa fadhila wateja wake waaminifu.

Kimori alisema vile vile promosheni ya MastaBata – Kivyako Vyako inatoa fursa kwa wateja wanaofurahia huduma za malipo ya kadi huku ikiwapa nafasi ya kushinda fedha zitakazofanya msimu huu wa Krismasi na Mwaka Mpya kufana.

Alisema kwenye kampeni hiyo zawadi zitatolewa kwa washindi zaidi ya 1,000 ambao kati yao 100 watapatikana kila wiki, 25 kila mwezi na wale 30 wa kuhitimisha kampeni watanyakua Sh. milioni tatu kila mmoja.

# Makaburi 200 Vingunguti kuhamishiwa Chanika

**Na Christina Mwakangale**

HALMASHAURI ya Jiji la Dar es Salaam, imesema inaanza kuyahamisha makaburi 200 yaliyoko Vingunguti, leo, ikisema ni kutokana na kusombwa na maji ya Mto Msimbazi, unaokatiza eneo la makaburi hayo.

Imesema makaburi hayo yanahamishiwa Mwanagati, Chanika jijini Dar es Salaam, kwa siku tatu mfululizo, bila kuwapo fidia.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Mashauri, alisema hatua hiyo ni kuwasaidia wananchi wa eneo hilo ambao ndugu zao walizikwa hapo na kwamba kila mvua inaponyesha, makaburi husombwa.

"Sio kwamba eneo hili tunalihitaji kwa ajili ya kuliendeleza, mto umekula hakutakuwa na fidia, tunawasaidia wananchi, ili kuhifadhi miili hiyo ambayo inakwenda na mto. Tunapeleka maeneo ya Mwanagati, Chanika. "Mto Msimbazi unaongezeka, wiki mbili, tatu zilizopita iliponyesha ilizoa makaburi," alisema mkurugenzi huyo.

Mashauri alisema uharibifu unaotokana na mto huo, ni mkubwa na kuna wakati baadhi ya majeneza huonekana ikiwamo nguo za marehemu.

Kadhalika alisema, fidia ya kuhamisha makaburi hulipwa kama eneo linatakiwa kupisha mradi, akisema Vingunguti hakuna mradi wowote utakaofanyika.

Alisema hatua hiyo huchukuliwa iwapo kuna dharura na si mara ya kwanza kufanyika, akisema mwaka jana kipindi cha mvua waliyaondoa makaburi mengine nane.

Vile vile, Ofisa Afya wa Halmashauri ya Jiji, Reginald Mlay, alisema kwa sasa unafanyika utengenezaji majeneza ili kuhifadhi mabaki ya miili hiyo.

Aliwataka ndugu watoe ushirikiano ili shughuli hiyo iweze kutekelezeka kirahisi na wanatarajia kukamilisha kazi katika muda uliopangwa.

Nimzihirwa Mjema, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Butiku, alisema hatua hiyo ni nzuri kwa kuwa kimekuwa kilio cha muda mrefu kwa wananchi wa mtaa huo.

"Tatizo hili limetokana na kupanua Mto Msimbazi, ambao unasababisha mafuriko. Ndugu za miili ya watu 180 wameshajitokeza na kujiandikisha," alisema Butiku.

# Waziri wa Afya akutwa na UVIKO-19

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI idadi ya watu walipata maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19 ikiendelea kuongezeka, Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, ametangaza kupata maambukizi ya ugonjwa huo.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Mazrui alisema kuwa kwa sasa hali yake ya kiafya inaendelea vizuri huku akiendelea kufuata masharti ya wataalamu wa afya ili kutoeneza virusi hivyo kwa watu wengine.

Mazrui alisema alibainika kuwa na ugonjwa huo Desemba 24 baada ya kwenda kupimwa hospitalini na kwamba amejitenga nyumbani kwake.

"Siku ya Alhamisi nilianza kujisikia homa kali mafua, kuharisha nilienda hospitali kupima nikakutwa na maambukizi kwa hiyo kwa sasa nimejitenga nyumbani siendi kazini mpaka kipindi cha wiki moja niangalie hali itakavyokuwa," alisema.

Alisema kuwa chanjo alizopata zimemsaidia afya yake kwa sababu ugonjwa huo haujamwangusha na kuwasisitiza wananchi kutodharau kupata chanjo hiyo.

Alisema hata mtu akienda kumtembelea nyumbani kwake kwa sasa wanaongelea dirishani ili kuepusha kusambaza maambukizi ya ugonjwa huo.

Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari zote dhidi ya ugonjwa huo na kuchanja akisema hata yeye chanjo ndiyo imempunguzia makali ya ugonjwa huo.

"Ugonjwa upo na watu wanaumwa, lakini hawaendi hospitali kupimwa na kupata matibabu, wengi wanabaki nyumbani na kujitibu wenyewe, tutoke twende hospitalini, lakini wananchi waendelee kunawa mikono, kuvaa barakoa na kuacha mikusanyiko isiyo ya lazima," alisema Waziri Mazrui.

Hadi Desemba 24 watu 89 wamegundulika kuwa na dalili za maradhi ya UVIKO-19 wakiwamo madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Rufani Mnazimmoja.

Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Marijani Msafiri, akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu hali ya ugonjwa huo katika ofisi zake Mnazimmoja, alisema wagonjwa hao ni kati ya 143 waliofanyiwa kipimo cha UVIKO-19 kuanzia Desemba 16, mwaka huu hadi Desemba 24.

Alisema kati ya wagonjwa 89 wafanyakazi, madaktari na wauguzi wa hospitali waliopatikana na UVIKO-19 ni 38.

Virusi vya corona vya UVIKO-19 ni mlipuko mpya uliogunduliwa mwaka 2019. Dalili zake ni pamoja na homa, kikohozi, shida katika kupumua, na katika hali ngumu zaidi, maambukizi yanaweza kusababisha, nimonia, kukosa pumzi, kushindwa kufanyakazi kwa figo na hata kifo.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Sofia Jongo, akionyesha silaha aina ya gobore zilizokamatwa juzi baada ya jeshi hilo, kufanya msako na kukamata vitu mbalimbali. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Samia atuma rambirambi kifo cha Askofu Mwenisongole

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametuma salamu za rambirambi kutokana na kifo cha aliyekuwa Askofu Mkuu wa Kanisa Tanzania Assemblies of God (TAG), Askofu Dk. Ranwell Mwenisongole.

Rais Samia alituma salamu hizo jana kupitia ukurasa wake Twitter.

"Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Askofu Dk. Ranwell Mwenisongole aliyekuwa Askofu Mkuu wa Awamu ya Pili ya TAG. Pole kwa familia, Askofu Mkuu Dk. Barnabas Mtokambali, wana TAG wote, ndugu, jamaa na marafiki. Mwenyesi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amina."

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, Dk. Barnabas Mtokambali, Askofu Mwenisongole anatarajiwa kuzikwa Desemba 30, mwaka huu, Vwawa wilayani Mbozi, mkoani Songwe.

Taarifa hiyo ilisema Askofu Mwenisongole alifariki juzi kwa mshtuko wa moyo na alikuwa akisumbuliwa na kisukari na shinikizo la damu.

Ibada ya kuaga mwili inatarajiwa kufanyika Desemba 29, katika Kanisa la City Christian Center, Upanga jijini Dar es Salaam.

Akieleza wasifu wake, alisema Askofu Mwanisongole atakumbukwa kwa mengi ikiwamo uongozi wake wa ushupavu, kwa kanisa hilo kwa kipindi cha miaka 16 akiwa Askofu Mkuu wa kanisa hilo tangu mwaka 1992 hadi mwaka 2008.

Alisema katika kipindi cha uongozi wake, kanisa hilo lilipata heshima kubwa na aliimarisha mfumo wa elimu ya theolojia na kuhimiza wachungaji kujiendeleza kielimu.

Pia, alisema maendeleo mengi katika kanisa hilo yalipatikana katika kipindi cha uongozi wake.

"Askofu Mwenisongole alikuwa anasumbuliwa na tatizo kisukari na shinikizo la damu, alikuwa chini ya uangalizi wa madaktari mpaka mshtuko wa moyo uliposababisha kifo chake, kwa sasa msiba upo nyumbani kwake mbezi beach Makonde," alisema Dk. Mtokambali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Walinda usalama viwanjani acheni vipigo kwa mashabiki

**MOJA** kati ya matukio yaliyowashangaza wengi kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya KMC na Simba, iliyopigwa katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora, ni mlinda usalama kumpiga mateke shabiki mmoja aliyevuka eneo la kukaa mashabiki kwenda kutaka kushangilia bao la nne pamoja na wachezaji.

Ilikuwa ni baada ya Kibu Denis kufunga bao la nne, na kisha mshambuliaji huyo kukimbilia sehemu ambayo ina mashabiki wengi wa Simba kushangilia karibu yao, lakini kutokana na furaha iliyopitiliza, mashabiki wawili waliruka chini kutoka jukwaani walipokuwa wamekaa na kisha kuwafuata wachezaji kushangilia pamoja.

Lakini kilichotokea hapo ni kipigo alichokipata mmoja wao aliyekuwa amevaa jezi ya Simba, na aliyebaki ilibidi arejee alikotoka kwa kuhofu yasije kumkuta kama mwenzake.

Kamwe, hatuwezi kuwa sehemu ya kuhamasishi mashabiki wa soka kuingia uwanjani wakati mechi ikiendelea, au bao linapofungwa, kwa sababu hairuhusiwi kufanya hivyo, na ni kitu ambacho hakikubaliki, ndiyo maana kwenye viwanja vyote duniani kumekuwa na walinzi wanaofanya kazi hiyo ya kuwalinda wachezaji wasivamiwe na mtu yeyote yule ili soka lichezwe bila bughudha yoyote.

Pamoja na hayo duniani kote matukio ya mashabiki au wanyama kuvamia uwanja haviepukiki uwanjani, na huwa vinatokea, ingawa kwa nadra sana. Hata hivyo, tumekuwa tukishuhudia namna wenzetu kwenye michuano mbalimbali barani Ulaya tukio kama hilo likitokea, walinzi kazi yao inakuwa kumkimbilia mhusika huyo na kumkamata kisha kumtoa bila kumuadhibu na mechi kuendelea.

Shirikisho la Soka Duniani (Fifa) liliamua watu wanaolinda usalama viwanjani wasiwe askari polisi au mgambo, badala yake ni walinzi maalum ambao wamepata mafunzo kutoka kwenye vyama vya soka na si vinginevyo, hivyo kilichotokea Ijumaa iliyopita tunaamini Shirikisho la Soka nchini (TFF), sasa litakifanyia kazi kwa kuwakumbusha walinda usalama kutotoa vipigo vikali kwa mashabiki wa soka mithili ya mbwa mwizi.

Aliyekuwa anampiga shabiki yule alimchukulia kama mhalifu na si shabiki wa soka aliyekumbwa na mhemko tu kutokana na timu yake kupata ushindi. Alichopaswa kufanya mlinzi yule ni kumkamata na kumrudisha alikotoka kwa sababu yule ni mteja na si mhalifu.

Zama za kuwachukulia wanaokwenda mpirani kuwa ni mashabiki tu wa soka badala ya wateja kama zilivyo biashara zingine zozote zimekwisha, hivyo huu ni wakati wakuwalinda na kuwaheshimu hasa inapoaminika hana dhamira mbaya ya kuhatarisha usalama.


TFF na klabu zinatumia gharama kubwa kuhamasisha mashabiki kwenda viwanjani ili kunufaika kimapato, lakini kama itaanza kuonekana au kuzoeleka kuwa shabiki anapopandwa na mzuka anafanyiwa kama yale aliyoyafanya kijana huyo kwenye mechi ya KMC FC dhidi ya Simba, basi watazidi kupungua uwanjani kila uchao.

Haikuhitaji kuwa na shahada ya sayansi ya roketi ('bachelor degree in rocket science) ili kumtambua kwamba shabiki yule hakuwa hatari au na athari yoyote ile. Kwanza alikuwa amevaa jezi ya Simba kwa hiyo isingewezekana kwamba anakwenda kuwadhuru wachezaji wao, hivyo angeweza kudhibitiwa kwa urahisi na kurudishwa alikotoka bila kupigwa. Hivyo tunakemea vikali matumizi makubwa ya nguvu na vipigo kwa mashabiki kutoka kwa walinda usalama viwanjani.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ligi ya Wanawake nayo iangaliwe zaidi

Na Adam Fungamwango

LIGI Kuu ya Soka ya wanawake Tanzania Bara, ilianza Alhamisi iliyopita kwenye viwanja mbalimbali nchini, ikizihusisha jumla ya timu 12 zinazochuana kutafuta bingwa atakayeiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa mwakani.

Mabingwa watetezi, Simba Queens, wakaanza kwa kishindo baada ya kuibamiza bila huruma Ruvuma Queens kwa mabao 15-0 kwenye Uwanja wa Mo Arena.

Watani zao wa jadi, Yanga Princess nao hawakuwa nyuma, wakaanza kwa kishindo kwa kupata ushindi wa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

Kwenye Uwanja wa Nyamagana. wenyeji, Alliance Girls walianza ligi kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mlandizi Queens.

Timu ya Fountain Gate Princess iliishikisha adabu Ilala Queens kwa mabao 4-0, kwenye uwanja wao wa nyumbani, wakati katika Uwanja wa Meja Isamuyo, Maafande wa JKT Queens waliisasambua Oysterbay Girls mabao 3-1.

TSN Queens, ikiwa nyumbani, Uwanja wa CCM Kirumba ilikiona cha moto, ilipochabangwa mabao 4-0 dhidi ya The Tigers Queens.

Ni ligi iliyoanza bila mvuto sana kama ilivyokuwa msimu uliopita, labda kutokana na kuwapo kwa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Inawezekana kabisa kuwa msimu huu haikuwa na matangazo makubwa kama msimu uliopita, ambapo baadhi ya mechi zilikuwa za kusisimua.

Tuliona mechi moja ya Simba na Yanga iliyoonyeshwa moja kwa moja kwenye televisheni, ilivyokuwa ya ushindani mkubwa uwanjani na hata nje ya uwanja, mashabiki wakiwa wamefurika kama vile mechi ya soka la wanaume.

Na hii ilileta hamasa kubwa kwa wachezaji wenyewe na kujikuta wakijituma na kuona fahari kuzitumikia timu zao, lakini wakiona soka la wanawake sasa limekuwa na thamani.

Kwenye mechi za mwishoni kuelekea kwenye ubingwa wakati Simba Queens na Yanga Princess zikifukuzana kuwania ubingwa, mashabiki walikuwa wakifuatilia matokeo ya ligi hiyo kwenye televisheni, redio na hata mitandao ya kijamii kujua nani kashinda na yupi mwenye pointi na magoli mengi na hata wanaofukuzana kuwania ubingwa.

Mechi za mwisho wakati Simba ikicheza mkoani, Yanga Dar es Salaam, mashabiki wa soka walikuwa wakiulizana na kujuzana matokeo kwenye mitandao ya kijamii, kiasi kwamba Yanga Princess ilionekana kama itatwaa ubingwa, lakini bao la dakika ya mwisho la Simba mjini Dodoma, likawapa ubingwa.

Kama itakumbukwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan tayari amejitolea kudhamini soka la wanawake kwa klabu Ukanda wa CECAFA baada ya kuona kuwa halikuwa na mdhamini yeyote, huku lile la wanaume likidhaminiwa na Rais wa Rwanda, Paul Kagame.

Kwa sasa klabu bingwa ya Afrika Mashariki na Kati ya wanaume na ya wanawake yote yana wadhamini.

Nilidhani sasa hapa Tanzania kampuni nazo zingeunga mkono juhudi za Rais kuinua soka la wanawake kuweka udhamini wao kama inavyoonekana kwenye soka la wanaume.

Tumeona hivi karibuni mgogoro wa baadhi ya kampuni kugombania kuwekwa nembo kwenye bega, kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara wanaume, huku kukiwa na kampuni nyingine pia, lakini kuna uhaba mkubwa wa wadhamini kwenye soka la wanawake.

Shirikisho la Soka nchini (TFF), kitengo cha biashara ni kama vile wanajitahidi kusaka wadhamini kwa wanaume, hivyo wafanye hivyo hivyo kwa wanawake.

Kwanza huko hakuna kelele na migogoro mingi, lakini kampuni zinaweza kujitangaza vizuri zaidi kwa pesa ndogo kuliko ambavyo wangefanya kwenye soka la wanaume.

Kuna kampuni ambazo zinazalisha au kutengeneza bidhaa za kinamama na watoto, nashangaa ziko kimya kujitokeza kwenye soka la wanawake.

Nadhani pia hata kitendo cha biashara ni wakati wa kuzifuata kampuni hizo na kuzieleza na kuzishawishi zitanufaika vipi na wadhamini ligi hiyo, huku pia wakijitahidi kuitangaza ligi hiyo kwa kuonyeshwa kwenye TV, hata kama ni kwa baadhi ya mechi hasa za Simba Queens, au Yanga Queens.




Muuguzi wa Zahanati ya Kwekivu, Loveness akitoa elimu ya chanjo ya UVIKO-19 kwa wajumbe wa Halmashauri ya Kata ya Kwekivu wakati wa ziara ya Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kilindi, Bakari Kingalangala, kikao kilichofanyika Sekondari ya Kwekivu. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Simiyu yaja na utaratibu mpya kunufaisha wakulima pamba

**Na Salome Kitomari**

MKOA wa Simiyu umekuja na mkakati wa kuweka mfumo shirikishi wa zao la pamba, utakaonufaisha wakulima moja kwa moja kwa kuondoa ujanja ambao umekuwa wa maumivu makali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Mkoa huo, David Kafulila, alisema mkoa huo unaongoza kwa uzalishaji wa pamba kwa miaka mingi na kuwa asilimia 40 hadi 50 ya zao hilo inayozalishwa nchini inatoka mkoani humo.

"Moja ya yaliyojitokeza kwenye zao hili ni kuwapo kwa wanjanja wanaokamata soko, tulikuwa tuna tatizo la baadhi ya watu kumiliki zao na kulifanya wanalotaka, moja ya kazi niliyofanya niliondoa kampuni mbili na ilisaidia kujenga nidhamu kwamba ukiharibu utaratibu unachukuliwa hatua, tumerudisha utaratibu wa ushindani na wakulima wakapata bei nzuri," alisema.

Kwa mujibu wa Kafulila, mkulima akiwa na uhakika wa bei anaongeza bidii na ndiyo maana mkoa huo umekuja na muundo unaohusisha wakulima kuanzia ngazi ya kijiji hadi mkoa ikiwa na nusu ya serikali na sekta binafsi, baada ya kubaini kuwa wananchi wanakosa mkono wa serikali.

"Tofauti yake na tulikotoka ushirika ngazi ya kijijij ndiyo walikuwa wasimamizi wa zao la pamba na kulikuwa na upigaji mwingi, uwajibishaji mdogo na kila wakitaka kuchukuliwa hatua wanasema sisi ni ushirika, tunajitegemea, wanajihisi wana kinga kwamba mambo yao wamalize wenyewe," alifafanua Kafulila.

Alisema kutatua hilo ndiyo maana wakaja na mfumo wenye serikali kwa maana ya Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kijiji ambaye ni wa serikali, ambayo itasaidia kuongeza ushiriki wa serikali na kuondoa utawala wa vyama vya msingi na mwisho kumnufaisha mkulima.

Alisema muundo huo utatumika kwenye kugawa mbegu na ununuzi Mei mwakani, na kwamba lengo ni kumpa mkulima ujasiri kwa kuwa ushirika ni nguzo ya kusimamia kilimo, lakini kuna virusi vinavyopaswa kushughulikiwa kutokana na mkulima kuumia.

Kwa mujibu wa Kafulila, asilimia 80 ya wakulima sio wanachama wa ushirika, lakini sheria inawataka lazima wauze kupitia ushirika na kwamba kuna gharama wanakatwa za AMCOS, Ushirika mkoa, Bodi ya Pamba na Tume ya Ushirika Tanzania bila kujali kwamba mkulima alipewa huduma yoyote jambo ambalo ni maumivu kwa mkulima.

"Lengo langu ni wakulima wabaki ndani ya ushirika waimarishe ili kuwakabili wajanja, pia nimeshauri uanachama wa ushirika kwenye pamba, shamba la mkulima liwe mwanachama na kwamba kama anakatwa makato yote hakuna haja ya kusajili na kulipia kuwa mwanachama," alifafanua.

"Msimu uliokwisha kutokana na ongezeko la hamasa na kuhusisha wakulima wafuate taratibu za kilimo mafanikio ni kufikia asilimia 61 ya pamba Tanzania na hii ni mara ya kwanza, msimu uliokwisha pamba yote nchini ilikuwa tani 140, 000 au kilo milioni 140, ila msimu huu pekee imezalisha kilo miloni 81," alisema.

Kwa mujibu wa Kafulila, pamba ni dhahabu ya Simiyu (white gold) kwa kuwa inachangia sehemu kubwa ya maisha ya watu wa mkoa huo, mchango wake kwenye nchi ndiyo wanachojivunia, na kwamba historia ya zao hilo linalimwa kama sehemu ya mila hata likitokea jambo lolote wanaendelea kulima.

Alisema kwa mwaka huu kuna mafanikio makubwa kwa kuwa kwenye kumbukumbu za bodi ya pamba kwa zaidi ya miaka 30 haijawahi kutokea bei nzuri kama ya mwaka huu ambayo ilikuwa ni Sh. 1,800 kwa kilo huku miaka mingine ilikuwa 1,200.

"Hii inaonyesha kuna bidii imefanyika kwasababu kwanini mwaka huu bei ilipanda, lakini haikufika dola moja, lakini mkulima amepata bei ya juu, tunaona haya ni mafanikio ya kiusimamizi kwamba tuondoe ujanja ujanja kwenye zao hilo," alisema.

Aidha, alisema mkakati mwingine ni kufufua viwanda vitatu vya kuchambua pamba ambavyo havihitaji marekebisho makubwa na tayari kuna uwezekano wa kuviwezesha kufanyakazi.

Alisema lengo ni kuhakikisha wakulima wanamiliki ushirika na kupunguza unyonyaji huku akitolea mfano kwa mwaka huu Bodi ya Pamba ilipata Sh. bilioni 21 mkoani humo ikiwa ni Sh. 250 kwa kilo milioni 81 na wakulima walipewa pikipiki za Sh. milioni 178 jambo ambalo sio sahihi.

"Kama lengo la ushirika ni kukabili unyonyaji wa soko kwa kuamini ushindani unaumiza ila mfumo hauwezi kuwa wa kuchukua Sh. bilioni 21 na kurudisha Sh. milioni 178, kwa muundo huu kilimo hakiwezi kwenda," alisema.

# Watembea kilomita 28 kusaka huduma za afya

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa vijiji vya Mbatamila, Kitalo na Nampungu, Kata ya Nampungu wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, wanalazimika kutembea umbali wa kilomita 28 kufuata mahitaji na huduma mbalimbali za kijamii zikiwamo za afya.

Kadhia hiyo inatokana na kuharibika kwa barabara inayoanzia kata jirani ya Nandembo hadi Nampungu na kusababisha magari ya abiria kusitisha safari, hali inayowalazimu wananchi wa vijiji hivyo kutumia usafiri mbadala kufika katika vituo vya afya.

Wakielezea kero hiyo kwa Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Hassan Kungu, wananchi wa maeneo hayo walisema barabara hiyo kwa sasa imeharibika na kuwa mashimo makubwa yaliyosababishwa na mvua zilizonyesha miaka miwili iliyopita na kuachwa bila kufanyiwa matengenezo.

Rashid Mwakambaya, aliiomba serikali kupitia Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), kufanya matengenezo ya haraka ya barabara hiyo kabla ya mvua za masika hazijaanza ili waweze kuitumia katika shughuli za maendeleo ikiwamo kusafirisha mazao kwenda sokoni.

Mwajuma Ali alisema kuharibika kwa barabara hiyo kunawatesa wajawazito wa vijiji vinavyounda Kata ya Nampungu kushindwa kwenda hospitali.

Diwani wa Kata ya Nampungu, Jaffar Fundi, alisema endapo serikali itachelewa kuchukua hatua za haraka, upo uwezekano wa kukatika kwa mawasiliano kati ya vijiji vya Kata ya Nampungu na maeneo mengine.

Aliwataka wananchi wa kata hiyo kuwa na utaratibu wa kujitolea nguvu zao na kushiriki katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo badala ya jukumu hilo kuiachia serikali.

Alisema licha ya Kijiji cha Nampungu kuanzishwa kwa muda mrefu, bado kipo nyuma kimaendeleo kutokana na wakazi wake kusuasua katika suala la kujitolea nguvu na fedha na kusababisha kuchelewa kwa maendeleo.

Mbunge huyo alisema serikali imeshatoa Sh. milioni 450 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe, ili iweze kupitika na wananchi waitumie kusafiri na kusafirisha mazao hasa maarufu la korosho kwenda katika minada.

Kungu, aliwaomba wananchi hao kuunga mkono jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali.

Meneja wa TARURA, Wilaya ya Tunduru, Silvanus Ngonyani alisema, mkandarasi kampuni ya MS Mucha Bulding Ltd alitakiwa kuanza kazi tangu Desemba 6, mwaka huu, lakini hadi sasa hajafika eneo la mradi kutokana na changamoto ya kifedha.

## HABARI PICHANI













Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakiwa katika mapumziko ya Boxing Day ufukwe wa Coco Oysterbay jana. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**

HABARI KITAIFA

# Kliniki ya tohara tembezi kuelimisha chanjo UVIKO-19

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imezindua huduma ya kliniki tembezi ya tohara itakayokuwa inatolewa bure kwa vijana wenye umri wa miaka 15 na kuendelea ikiwa pamoja na utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 kwa watakaokuwa wanafika kupatiwa huduma hiyo.

Lengo la kuanzisha huduma hiyo ni kudhibiti maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na kutoa elimu ya chanjo ya Uviko-19 katika kata 20 zinazounda halmashauri hiyo na kuondoa msongamano wa vijana na watu wazima wanaofika kupata huduma.

Mpango huo umefadhiliwa na Mfuko wa Rais wa Marekani (PEFPAR) chini ya CDC kuendelea kupambana na maambukizi mapya ya Ukimwi kwa vijana balehe na watu wazima ambao hawajafanyiwa tohara.

Hayo yalibainishwa juzi na Mratibu wa huduma za tohara Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Dk. Hajji Swedi wakati wa uzinduzi wa huduma ya kliniki tembezi kuwa, vijana balehe na wanaume ambao hawajapata tohara wanatakiwa kujitokeza huduma hiyo itakapowafikia katika kata zao.

Alisema, tohara ina manufaa makubwa katika mwili wa mwanadamu kwa sababu inakinga maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kwa asilimia 60 kwa wanaume na kumkinga mwanamke na saratani ya mlango wa shingo ya uzazi na kwamba zoezi hilo litatolewa hadi ngazi za kata. "Huduma hii itakuwa inatembea kuzunguka kata zote 20 za manispaa yetu ya Kahama, na zitatolewa na wataalamu waliopata mafunzo maalumu ya kutosha na huduma zote zitakuwa zinatolewa bure bila malipo, tohara na chanjo ya UVIKO-19," alisema Swedi.

Naye mdau wa afya, Chalo Charido alisema, wamekuwa wakitoa huduma ya tohara kwa vijana wenye umri wa 15 na kuendelea, lengo likiwa ni kupambana na VVU ambavyo vimeshamiri na kusababisha Mkoa wa Shinyanga kuwa miongoni mwa inayoongoza kitaifa kwa maambukizi.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Dk. Lucas David alisema, huduma hiyo imesaidia kupunguza msongamano wa wateja waliokuwa wakifika hospitalini kupata huduma hiyo na watawafikia wengi zaidi hasa kata zilizoko pembezoni.

David alisema, uwapo wa huduma hiyo utasaidia kuendelea kutoa elimu na utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 kwa wananchi walioshindwa kufika katika vituo vya afya kupata chanjo kutokana na uwepo wa sababu mbalimbali na kuwataka wananchi watakao ona huduma hiyo wajitokeze.

Mmoja wa wateja waliojitokeza kupata huduma ya tohara Baraka John alisema, huduma hiyo itasaidia kupunguza adha ya kutembea umbali mrefu kufika katika vituo vya afya kupata huduma na kwamba awali waliikosa baada ya kukuta msongamano wa wateja hospitalini.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mjini, Mohamed Moyo, akikagua ujenzi wa madarasa ya sekondari yaliyotumia fedha za UVIKO-19, juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Tanga yabaini mbinu kupunguza ajali barabarani

**Na Steven William, MUHEZA**

KAMANDA wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Tanga, Leopord Fungu, amesema ukaguzi wa mabasi ya abiria kutoka mkoa huo kwenda mikoani ni endelevu.

Alisema kikosi hicho kinafanya ukaguzi wa mabasi hayo kipindi chote cha sikukuu na ukaguzi huo utakuwa endelevu ili kuepuka ajali.

Alisema hayo juzi wakati akikagua mabasi hayo kutoka Tanga mjini kwenda mikoani stendi kuu ya mabasi na stendi kuu ya Muheza na Korogwe.

Alisema mabasi yanayogundulika kuwa mabovu yanazuiliwa kuendeleza na safari.

Kamanda huyo alisema, kuwa Jeshi la Polisi pia linatoa elimu kwa abiria ndani ya mabasi kufahamu wajibu kuhusu usalama wao.

Alisema kuwa zoezi hilo la ukaguzi wa mabasi makubwa na madogo ni endelevu na limesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ajali.

Katika hatua nyingine aliwasisitiza abiria wanapoona dereva anakwenda mwendo kasi watoe taarifa kwa vyombo vya usalama.

Pia, alitoa tahadhari kwa abiria kuwa waangalifu wanapokuwa ndani ya basi kwa kutokubali kupewa vinywaji ama chakula na abiria mwenzake kwa kuwa wengine wana nia mbaya ya kuwaibia abiria.

Aliwakumbusha abiria kujenga utamaduni wa kufunga mikanda kwa ajili ya usalama wao panapotokea ajali iwakinge wasipate madhara makubwa.

# Wanawake kuendesha mitambo Mgodi Bulyanhuru

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MGODI wa dhahabu Bulyanhuru, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, umetangaza ajira kwa wanawake kuendesha teknolojia mpya ya uchimbaji wa madini na ulipuzi wa miamba ya dhahabu chini ya ardhi kwa kutumia njia ya kompyuta.

Awali, shughuli hiyo ilikuwa inafanywa na wanaume kwa asilimia kubwa na wakati wa ulipuzi huo mgodi husimamisha uzalishaji kwa muda wa saa mbili hali inayosababisha hasara kwa mwekezaji wao.

Mhandisi Mwandamizi wa mgodi huo, Edwin Bashasha, alisema hayo wakati akitoa taarifa ya shughuli ya uchimbaji wa madini kwa Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, alipofanya ziara ndani ya mgodi huo kujionea shughuli mbalimbali za uzalishaji.

Alisema, wameanzisha teknolojia mpya ya uchimbaji wa madini mwezi Aprili mwaka huu na unatarajia kukamilika mwakani mwezi Juni na watakaoendesha ni wanawake ili kuwashirikisha katika shughuli za uchimbaji wa madini.

Bashasha alisema, teknolojia hiyo itasaidia kuongeza uzalishaji, usalama wa watumishi kazini na kuongeza ajira kwa wanawake na kwamba tatizo lililopo kwa sasa ni wingi wa joto lililopo chini ya ardhi na baadhi ya miamba kuanguka na kuleta maafa kwa wafanyakazi.

"Tunapoteza muda wa saa mbili wakati wa ulipuaji wa miamba ya madini ardhini, tunatoa wafanyakazi wetu wote shimoni kwa wakati huo na hii ndiyo sababu kubwa ya kuanzisha teknolojia hii ambapo ikitokea tatizo ardhini itaharibu mitambo pekee," alisema Bashasha.

Naye Waziri Biteko aliwapongeza kwa kuanzisha teknolojia hiyo ya uchimbaji madini kisasa na kwamba migodi mingi iliyopo duniani wanatumia mifumo hiyo katika shughuli za uchimbaji na ulipuaji wa miamba ya madini ardhini.

Alisema, kilichomfurahisha zaidi ni kusikia watakaoendesha mifumo hiyo katika uchimbaji wa madini kwa kutumia njia ya kompyuta ni wanawake na Rais Samia Suluhu Hassan anapenda kuona rasilimali za nchini hasa madini zinawanufaisha watu wote. Dk. Biteko alisema, awali wanawake walikuwa hawaruhusiwi kwenda katika maeneo ya migodi kwa kisingizio madini hayapatikani na ilikuwa dhana mbaya ambayo ilikuwa inawabagua wanawake, lakini kwasasa wanamiliki maduara ya uchimbaji na leseni, na madini yanapatikana kwa wingi.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Msalala Iddi Kassimu alisema, halmashauri imepokea Sh. bilioni 2.5 fedha zinazotengwa na wawekezaji kwa ajili ya maendeleo (SCR) kutoka mgodi huo na kwamba Sh. milioni 400 zitajenga chuo cha uuguzi, Sh. milioni 400 maegesho ya magari Isaka, Sh. milioni 12.2 kujenga kituo cha mabasi Segese na Sh. milioni 20, Chuo cha Veta Bugalama.

# 'Madume' watatu wazaliwa mkesha Krismasi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATOTO wa watatu wa kiume wamezaliwa katika mkesha wa Sikukuu ya Krismasi katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga.

Muuguzi Msaidizi Kiongozi wodi ya wazazi, Experantia Misalaba, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari hospitalini hapo.

Alisema kinamama waliojifungua kwenye mkesha wa Sikukuu ya Krismasi ni watatu, wawili wamejifungua kwa njia ya upasuaji na mmoja kawaida, na wote wapo salama, wakiwa wamejifungua watoto wa kiume wenye afya njema.

"Tumefarijika kinamama hawa kujifungua salama, hasa hawa wawili ambao wamejifungua kwa njia ya upasuaji, ni jambo jema kwetu kuona tunapunguza vifo vitokanavyo na uzazi, natoa wito kwa wanawake waje kujifungua hospitali sehemu ambayo ni salama," alisema Misalaba.

Mmoja wa kinamama hao aliyejifungua kwenye mkesha huo, Lightines Kadala, mkazi wa Kitangili Manispaa ya Shinyanga, alisema anamshukuru Mungu kujifungua mtoto wake salama pamoja na yeye kuwa na afya njema.

"Nina furaha sana sababu Yesu amezaliwa na mimi nimejifungua siku hiyo hiyo tena mtoto wa kiume, nilikuwa nikimwomba Mungu nijifungue siku kama ya leo na imekua hivyo, na tayari mtoto wangu nimeshampatia jina la Emmanuel," alisema Kadala.

Kwa upande wake Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto mkoani Shinyanga, Joyce Kondoro, akizungumza na Nipashe wiki iliyopita, alisema ili kupunguza vifo vya uzazi, wanawake wanapaswa kuzingatia ushauri wa wataalamu, na kuhudhuria kliniki muda wote ili kupata vipimo na kujua maendeleo ya mtoto tumboni.

"Mjamzito anapokuwa akihudhuria kliniki mara kwa mara na kupata vipimo vya maendeleo ya mtoto wake ni vigumu sana kupoteza wakati wa kujifungua, tofauti na yule ambaye haji kliniki, na kuja hospitalini siku ya kujifungua, anakuwa katika hatari sababu hakuna historia yake, na mfano akihitajika upasuaji ndiyo mbaya zaidi," alisema Kondoro.

Pia, alitaja takwimu za miaka mitatu za vifo vya uzazi kwa upande wa kinamama mkoani humo, kuwa mwaka 2019 kulikuwa na vifo 50, mwaka 2020 (46) na mwaka huu 2021 vimepungua na kufariki kinamama 15.

Pia alitaja vifo vya watoto wachanga kuwa mwaka 2019 vilikuwa 866, mwaka 2020 (567), na mwaka huu vimepungua na kuwa 270, na kutoa wito kwa wajawazito, wanapokuwa wakijisikia vibaya wawahi hospitalini.




Mkuu wa Mauzo Vodacom Kanda ya Dar es Salaam na Pwani, Brigita Shirima (kushoto), akimkabidhi zawadi ya smart Tv mmoja kati ya washindi wa wiki ya tatu wa promosheni ya " Show Love, Tule Shangwe", Geofrey Nyakuka (kulia), mkazi wa Tabata, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Masta Shangwe, jumla ya washindi sita walijishindia Tv za kisasa (Smart Tv) wengine sita simujanja (smartphone) na washindi 50 walijishindia pesa taslimu. Ili uweze kushinda zawadi katika kipindi hiki cha sikukuu, mteja wa Vodacom unatakiwa kununua bando au kutumia huduma ya M-Pesa kwa kumpendae kwa kupiga *149 * 01#.

# Ataka madarasa ya UVIKO-19 yakamilike kwa wakati

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Chalinze, Hassan Mwinyikondo, amewataka makandarasi wanaotekeleza miradi ya UVIKO- 19 kufanyakazi kwa bidii kukamilisha kwa wakati.

Mwinyikondo alitoa wito huo juzi alipofanya ziara ya ukaguzi wa madarasa yaliyojengwa kwa fedha za UVIKO- 19, akiambatana wataalamu wa halmashauri hiyo kuona hatua iliyofikiwa kwa vyumba 80 vinavyojengwa.

Mwinyikondo alitembelea Shule ya Sekondari Kibindu, Kimange, Rupungwi, Changalikwa na shule shikizi ya Komtonga ambayo ilipelekewa Sh. milioni 320 kati ya Sh. bilioni 1.6 zilizotolewa kwa Halmashauri ya Chalinze kwa ajili ya madarasa 80.

Mwinyikondo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuisaidia halmashauri hiyo kutatua tatizo la upungufu wa madarasa. "Sikukuu ya Krismasi mimi, wataalamu na Kamati ya Ofisi ya Rais TAMISEMI tumetumia muda wetu kukagua miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, niwapongeze wasimamizi katika shule za

Moreto, Mboga, Chalinze, Msata, Miono na Vigwaza ambao wamekamilisha ujenzi kwa asilimia 100.

Mwinyikondo aliwaagiza wasimamizi na mafundi wa miradi hiyo kufanya kazi kwa bidii ili kuikamilisha kwa wakati na kufanikisha lengo kusudiwa ambalo ni kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mapema Januari 2022.

"Wito wangu kwa wasimamizi wa miradi hii kwa maana ya ofisi ya Mkurugenzi, Mhandisi wa wilaya, maofisa elimu (msingi na sekondari) na walimu wakuu, kamati za usimamizi fanyeni kazi usiku na mchana ili kuhakikisha lengo la kukamilisha miradi hii Desemba 28, linafikiwa," alisema.

Pia alimwagiza Ofisa Mipango kutafuta njia ya kupeleka fedha katika miradi kwa wakati hususani katika ujenzi wa vyoo kwenye shule zilizopata fedha za madarasa ya UVIKO-19.

## Kingalangala awatoa hofu makada CCM

**Na Dege Masoli**, KILINDI

MWENYEKITI wa CCM Wilaya ya Kilindi, Bakari Kingalangala, amewatoa hofu makada wa chama hicho wanaotaka kuwania nafasi ya mwenyekiti kwenye uchaguzi ujao wajipange na kwamba ziara yake haihusiani na kampeni kwa ajili ya uchaguzi huo.

Akizungumza na viongozi wa ngazi mbalimbali katika kata za Lwande, Kimbe na Negero, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya wiki mbili kukagua uhai wa chama na miradi inayotekelezwa wilayani humo na kusikiliza kero, Kingalangala alisema kutembea huko ni ahadi aliyowekeana na chama ya kila mwaka kuzunguka wilaya nzima.

Katika ziara hiyo aliambatana na viongozi mbalimbali ngazi ya wilaya akiwamo Katibu wa Madiwani, Juma Bewa, Mwenyekiti wa Wazazi, Amon Mhando, Katibu Msaidizi wa CCM, Pamphil James na madiwani viti maalumu, Habiba Mnguya na Hamida Kidunda na kada maarufu, Mohamedi Mkomwa.

Alisema kuwa ziara yake imekuwa mwiba kwa baadhi ya watu wanaotaka kuingia katika kinyang'anyiro cha uchaguzi hapo mwakani cha uenyekiti na kwamba wana wasiwasi kuona ni kampeni ya uchaguzi huo na kuwataka wasiwe na hofu.

"Ziara yangu inawapa watu shida sana, baadhi ya watia nia wanaifuatilia sana, kila ninapokwenda simu zinapigwa, watu wanauliza vipi? Kingalangala amepata watu hapo? Vipi amesemaje? Anapiga kampeni? Na mimi safari hii nimo, tumuangushe Kingalangala asichukue tena mara ya tatu!...Wanapata tabu sana," alisema Kingalangala.

Hata hivyo, aliwataka wasubiri muda utakapofika kila mwanachama anayo haki ya kugombea nafasi yoyote na kitendo cha kujenga hofu na ziara yake ni kutafuta kujiwekea vikwazo na kusisitiza kuwa cha msingi ni kusubiri muda ufike.

Alisema mwanasiasa mzuri ni yule anayenusa kila pembe kuona hali ya hewa ya kisiasa ilivyo vinginevyo kuingia kichwakichwa katika uchaguzi bila kuangalia, kunaweza kumfanya mtu kufutika kisiasa baada ya kuachwa mbali kwenye kura.

"Lakini mnaotaka kupambana na mimi mnuse kwanza, halafu je, mpo wangapi? Je, mtaweza?" Alihoji Kingalangala huku akisisitiza kwamba hapigi kampeni zaidi ya kuangalia utekelezwaji wa ilani, kusikiliza kero na kufuatilia miradi inayotekelezwa chini ya fedha za Uviko- 19 za Rais Samia Hassan Suluhu.

Mwenyekiti huyo anafanya ziara hiyo katika Kata 21 za Wilaya ya Kilindi na kukutana na viongozi wa halmashauri za chama ngazi ya kata, mabalozi, matawi, wazee maarufu na wataalamu, wakiwamo pia madiwani na kutoa maelekezo mbalimbali yanayohusu uimarishaji wa CCM.

Nipashe
Spotika




WACHEZAJI WA5 WENYE KADI NYEKUNDU NYINGI TANGU 2000 UK. 12 - 13




# WACHEZAJI WA5 WALIOKOSA PENALTI NYINGI KARNE YA 21

## ISIKUPITE

SIKU ya kufungua zawadi ('Boxing Day') Desemba 26, 1963 bado inaendelea kukumbukwa kwa matokeo ya kushangaza kwenye Ligi Kuu England baada ya Ipswich Town kupigwa mabao 10-1 na Fulham, huku Burnley ikiitandika Manchester United 6-1, West Brom ikitoka sare ta 4-4 dhidi ya Tottenham na Blackburn ikishinda 8-2 dhidi ya West Ham. Jumla ya mabao 60 yalifungwa siku hiyo.

**LONDON,** England

KWA mtazamo wa haraka, penalti inaonekana kuwa njia rahisi ya kufunga bao. Kumfunga golikipa kwa shuti la umbali wa yadi 12 kunaweza kuchukuliwa kama matembezi kwenye bustani, haswa kwa wafungaji bora duniani.

Lakini, unapozingatia uzito wa matarajio na uzuri wa makipa, hali inakuwa ngumu zaidi. Hawa ndio wachezaji watano bora ambao wamekosa penalti nyingi zaidi karne hii ya 21...

### #5. Antonio Di Natale – Penalti 14

Gwiji wa Udinese, Antonio Di Natale alikuwa mmoja wa wachezaji bora kabisa katika kipindi chake. Tofauti na washambuliaji wengi wa kizazi chake, Di Natale hakutajwa sana alipokuwa kijana. Mshambuliaji huyo wa kati jina lake lilipaa baada ya kufikisha umri wa miaka 30.

Alikuwa na mguu mzuri wa kulia, alikuwa na harakati za kuvutia za nje ya mpira, na alikuwa na ustadi wa kuwa mahali pazuri kwa wakati muafaka. Kwa kuongezea, alikuwa mwaminifu kwa Udinese na alikataa ofa kutoka klabu nyingine za Serie A.

Di Natale aliifungia Udinese mabao 191 katika Ligi Kuu Italia, na kuwa mfungaji bora wa klabu hiyo. Di Natale pia ndiye mfungaji bora wa sita katika historia ya Serie A.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Italia alipiga penalti 55 katika maisha yake ya soka, akifunga 41 na kukosa 14. Alistaafu soka msimu wa joto wa mwaka 2016.

### #4. Zlatan Ibrahimovic - Penalti 16

Mpende au umchukie, hakuna njia ya kupuuza uwapo wake na uchezaji wa kuburudisha wa Zlatan Ibrahimovic. Mkali huyo wa Sweden amecheza katika klabu nyingi za juu barani Ulaya na anaendelea kutawala uwanjani hadi leo akiwa na AC Milan.

Kwa sasa ndiye mshambuliaji pekee mwenye umri wa miaka 40 anayeendelea kucheza mara kwa mara. Ameichezea Milan mechi 11 hadi sasa msimu huu, akifunga mabao saba.

Ukiacha mahojiano yake yaliyojaa kiburi, Ibrahimovic analeta mengi zaidi. Yeye ni mshambuliaji bora wa mpira, anaweza kushinda pambano la angani na ardhini kwa urahisi, na mara nyingi kwa kushangaza hana ubinafsi akikaribia lango.

Akiwa katika miaka yake 40, hafungi sana mabao yake ya sarakasi siku hizi, lakini amefunga machache ya kifahari.

Ibrahimovic amekuwa mpigaji penalti kwa timu zake. Katika kipindi cha uchezaji wake, amepiga penalti 100, akifunga 84 kati ya hizo na akikosa 16.

### #3. Francesco Totti - Penalti 18

Katika soka uaminifu umekuwa bidhaa adimu. Wachezaji kandanda hujitolea kubaki waaminifu kwa klabu zao, lakini huwa wanatafuta malisho mapya baada ya mizozo kidogo.

Gwiji wa AS Roma, Francesco Totti amekuwa tofauti na kawaida katika karne hii ya 21. Licha ya kupata ofa nyingi kutoka klabu nyingi za Ulaya ikiwamo Real Madrid, hakutaka kuondoka.

Kwa zaidi ya miaka 20, alikuwa mmoja wa majina ya kwanza kwenye karatasi ya timu ya AS Roma. Kwa kawaida kama mshambuliaji wa pili, Totti alikuwa na ustadi wa mkubwa. Alicheza mechi 618 za Serie A akiwa na Roma, akifunga mabao 250.

Wakati wake akiwa na Roma, alikuwa ndio mpiga penalti wa timu. Alipiga penalti 95 katika karne ya 21, akifunga 77 na kukosa 18.

### #2. Cristiano Ronaldo - Penalti 28

Mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo amekuwa mchezaji wa aina yake tangu alipoanza kucheza kwa mara ya kwanza katika kikosi cha kwanza cha Sporting Lisbon mwaka 2003. Mreno huyo amewahi kuzichezea pia Real Madrid na Juventus.

Ufungaji bora wa Ronaldo ulikuja wakati akiwa na wababe wa LaLiga, Real Madrid. Kati ya mwaka 2009 na 2018, nahodha huyo wa Ureno aliifungia klabu hiyo mabao 451, na kuisaidia kutwaa mataji mawili ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ronaldo amekuwa chaguo la kwanza la kupiga penalti katika kila timu aliyoichezea. Kufikia sasa, mfungaji bora wa kizazi hicho amepiga penalti 171 kwa klabu na nchi yake, akifunga mara 143 na kukosa mara 28.

### #1. Lionel Messi – Penalti 29

Mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Lionel Messi bila shaka ndiye mchezaji bora zaidi kuwahi kutokea duniani. Yeye ni mfungaji mabao wa kipekee na ameweza daima kuongoza kwa mfano kwenye uwanja wa mpira.

Kabla ya kuhamia PSG kwenye msimu wa majira ya joto wa 2021, Messi alikuwa ameichezea Barcelona pekee. Muargentina huyo alikuwa kwenye klabu hiyo kwa miaka 19, akihitimu kwanza kutoka akademi ya La Masia kisha akaibuka kama mchezaji bora wa kizazi chake.

Messi aliichezea Barcelona mechi 772 katika maisha yake ya soka, akifunga mabao 672 na asisti 301. Ushujaa wake akiwa Camp Nou ulimfanya kushinda Ballon d'Or sita. Alishinda Ballon d'Or yake ya saba akiwa PSG katika wiki ya mwisho ya Novemba.

Hadi sasa, Messi amepiga penalti 132, akifunga mara 103 na kukosa mara 29.

NIPASHE JUMATATU DESEMBA 27, 2021





# WACHEZAJI WA5 WENYE KADI NYEKUNDU NYINGI TANGU 2000


RAMOS

**LONDON,** England

MCHEZO wa soka haukomi kutushangaza kwa burudani na mapenzi yote yanayohusika. Inashangaza jinsi mashabiki kote ulimwenguni wanavyoufuatilia mchezo huo kama dini.

**Hiyo inasemwa, si mashabiki pekee ambao wanashauku kubwa juu ya mchezo huo. Shauku hutiririka kwa kasi pia kwa wachezaji wakiwa uwanjani.**

Kwa nguvu zote zinazohusika kwenye mchezo huo, wakati mwingine hutokea kwamba, wachezaji hupoteza udhibiti wao wenyewe. Wakati fulani, ni kwa namna ya makabiliano ya kimwili ambayo hatimaye husababisha mchezaji kutolewa nje. Wachezaji wanajulikana kuwa na mashambulizi makali na kuwahatarisha wachezaji wenzao wa upinzani.

Roy Keane alikuwa mmoja wa wachezaji wa mpira wa miguu wenye morali kubwa zaidi uwanjani wakati wake akicheza, kukabiliana naye ilikuwa ni kwa kutumia nguvu na hatari. Cha kushangaza raia huyo wa Ireland hayumo kwenye orodha hii ya wanasoka walioonyeshwa kadi nyekundu nyingi.

Makala haya inawaangalia wachezaji watano ambao wameonyeshwa kadi nyekundu mara nyingi zaidi katika ligi tano bora za Ulaya katika karne ya 21, twende sasa...

### #5. MATUZALEM (MARA 13)

Matuzalem alikuwa kiungo wa kati wa Brazil aliyechezea klabu nyingi za Ulaya katika maisha yake ya soka. Alicheza Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa muda mwingi zaidi.

Mbrazil huyo alizichezea Lazio, Brescia Calcio, Genoa, Piacenza Calcio, Napoli na Hellas Verona nchini Italia. Kwa mtindo wake wa uchezaji, Matuzalem alikuwa akipewa kadi nyekundu mara nyingi zaidi. Alitolewa kwa kadi nyekundu mara kumi kwenye Serie A.

Alipokuwa akiichezea Lazio, alitolewa nje mara moja kwenye Ligi ya Europa. Matuzalem alipokea heshima ya mashabiki kusimama mara mbili alipokuwa akiichezea Real Zargoza kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, ndani ya msimu mmoja tu.

### #4. ZLATAN IBRAHIMOVIC, GIAMPIERO PINZI, ALBERTO LOPO, SULLEY MUNTARI NA CYRIL JEUNECHAMP (MARA 14)

Nafasi ya nne inawakutanisha wachezaji watano kwa nafasi moja. Zlatan Ibrahimovic, Giampiero Pinzi, Alberto Lopo, Sulley Muntari na Cyril Jeunechamp wote wamekuwa na viwango tofauti vya mafanikio katika soka.

Ibrahimovic bila shaka ndiye aliyefanikiwa zaidi kati yao. Nyota huyo wa Sweden amekuwa na sifa mbaya uwanjani na haishangazi kwamba ametolewa nje mara 14 katika maisha yake ya soka. Ameonyeshwa kadi nyekundu mara tano akiwa na AC Milan, kadi nyingi zaidi katika klabu yoyote ambayo Zlatan ameichezea.

Pinzi alikuwa kiungo wa kati ambaye alicheza maisha yake yote nchini Italia. Alitolewa nje mara 13 akiichezea Udinese na mara moja Chievo Verona. Alberto Lopo alicheza maisha yake yote kule Hispania, kwa muda mrefu pale Deportivo de La Coruna na Espanyol. Alitolewa nje mara nne akiichezea Deportivo na mara nane akiichezea Espanyol.

Muntari siku zote alijulikana kwa kuwa na hasira za haraka na alitolewa nje mara 12 akicheza Serie A. Jeunechamp alicheza maisha yake yote ya klabu nchini Ufaransa kama kiungo wa kati wa ulinzi na alikuwa na mazoea ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu kutokana na uchezaji wake wa ukali.

### #3. GONZALO RODRIGUEZ (MARA 15)

Beki huyu wa kati wa Argentina alikuwa akicheza Villarreal baada ya kukaa kwa misimu tisa nchini Hispania. Katika muda huo, Rodriguez alitolewa nje mara nane.

Beki huyo mrefu wa kati alijiunga na Fiorentina kwenye Serie A mwaka 2012 na alikaa huko kwa misimu mitano. Jambo la kufurahisha ni kwamba, Rodriguez alitolewa nje mara mbili akiwa na timu hiyo ya Italia wakati wakicheza Ligi ya Europa. Katika ligi, alitolewa nje mara nne.

### #2. PHILIPPE MEXES NA THIAGO MOTTA (MARA 16)

Philippe Mexes alianza uchezaji wake huko Ufaransa akiwa na klabu ya Auxerre. Beki huyu wa kati wa Ufaransa amekuwa na sifa ya kupoteza udhibiti na kuwa mkali zaidi. Hii mara nyingi zaidi ilisababisha atolewe nje.

Akiwa Auxerre, alitolewa uwanjani mara moja tu. Ilikuwa pale AS Roma ambapo Mfaransa huyo alionyeshwa kadi nyekundu mara 11. Katika misimu minne iliyopita ya maisha yake ya soka, Mexes aliichezea AC Milan. Hata akiwa na miamba hao wa Italia, alitolewa nje mara tatu.

Thiago Motta alikuwa mmoja wa viungo wa kati waliokuwa hawatajwi sana. Kwa kutumia akili na uwezo wake wa kiufundi, alikuwa mtu wa kutegemewa katika safu ya kiungo. Lakini nyakati fulani, alipatikana na hatia ya kuwa mkali sana.

Katika maisha yake ya soka, Motta alitolewa nje mara tano akiwa na Paris Saint-Germain, mara nane akiwa na Barcelona, na mara moja akiwa na Inter Milan, Atletico Madrid na Genoa.

### #1. SERGIO RAMOS (MARA 26)

Sergio Ramos na kadi nyekundu zimekuwa zikienda naye sambamba. Beki huyo wa Hispania amekuwa mchezaji mzuri katika maisha yake yote ya soka na anaendelea kuwa mchezaji mkubwa uwanjani.

Pamoja na hayo, Ramos amekuwa mwepesi wa kupewa kadi nyekundu uwanjani. Kupenda kwake kuingilia ugomvi na timu pinzani na mara nyingi sana kumemfanya apewe kadi nyekundu. Mhispania huyo ana hadhi kubwa pale Real Madrid na cha kufurahisha, kadi zake zote nyekundu 26 alizipata wakati akiichezea timu hiyo.

Kati ya kadi hizo 26, 20 amezipata akiwa anacheza kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga. Ramos ana mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na ametolewa mara nne kwa kadi nyekundu katika michuano hiyo. Kadi nyekundu zilizobaki amezipata akicheza kwenye Kombe la Mfalme (Copa Del Rey).

Hakuna mchezaji mahiri anayeweza kumfikia Ramos linapokuja suala la kupewa kadi nyekundu mara kwa mara.

## Nukuu

"Hatukununua/hatutanunua mshambuliaji yeyote hivi karibuni ama baadaye. Siku moja itakwenda kutokea. Wakati iliposhindikana mwanzoni mwa msimu nilisema sawa, nimeridhika kwa kiasi kikubwa sana na wachezaji waliopo. Nitaishi nao hakuna tabu," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola**



"Kwa watu wengine wakisikia 'Messi' inamhusu mchezaji bora wa dunia, kwangu mimi ni jina la ukoo wangu, Cameroon watu wengi wana jina hili, utaona Messi wengi huko. Kwangu ni kawaida lakini kwa wengine si kawaida. Mara zote wanatarajia zaidi, wakisikia jina 'Messi'," **mshambuliaji wa Nanjing City F.C ya China, Mcameroon Raphael Messi Bouli**




"Watu wanasema ni nani mchezaji bora zaidi duniani? Na watu wengi wanasema kwa usahihi Messi - huwezi kupinga maoni hayo. Lakini Ronaldo anaweza kuichezea Millwall, Queens Park Rangers, Doncaster Rovers... mtu yeyote, na kufunga hat-trick katika mchezo mmoja. Sina uhakika Messi anaweza kufanya hivyo," **Kocha wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson akitoa maoni yake kuhusu nyota hao mwaka 2015**



# MAPEMA TU MAKOCHA 6 WAPUKUTISHWA LIGI KUU



Ndayiragije. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

MPAKA kufikia raundi ya 10 ya Ligi Kuu Tanzania Bara jumla ya makocha sita 'wameshatimuliwa' kwenye klabu wanazofundisha kutokana na sababu mbalimbali, lakini kubwa ni kutoweza kufikia malengo kwa timu zao kuanza kwa kufanya vibaya.

**Klabu nyingi kwa sasa zimekuwa zikiwatimua makocha wao kistaarabu kwa kile wanachodai ni wenyewe makocha kuandika barua ya kujiuzulu au kubwaga manyanga kwa maslahi ya pande zote mbili, lakini haiondoi ukweli kuwa hutimuliwa kutokana na matokeo mabovu.**

Msimu huu wa Ligi Kuu 2021/22, umeonekana ni mgumu na klabu nyingi zimekuwa hazina subira ya kuwapa muda makocha, badala yake huwaondoa pale wanapopoona mambo hayaendi vema.

Ikumbukwe kuwa msimu huu kuna timu 16 tu na kila timu itacheza mechi 30, hivyo kumekuwa hakuna muda wa kusubiri kwa makocha, mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, kila timu itakapokuwa imecheza mechi 15, tunaweza kuona ongezeko zaidi la makocha kutimuliwa.

Katika makala haya, tumekusanya orodha ya makocha wa timu za Ligi Kuu ambao tayari wameshapukutishwa kwa kuonyeshwa mlango wa kutokea, lakini aliyekuwa Kocha wa Simba, Didier Gomes hayupo katika orodha hii kwa sababu kutimuliwa kwake kulitokana na kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, twende sasa...

**ETIENNE NDAYIRAGIJE - GEITA GOLD**

Ni kocha wa zamani wa klabu za Mbao FC, Azam FC na timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars ambaye alichukuliwa na Geita Gold iliyopanda na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu huu.

Ilikuwa ni Agosti mwaka huu, Mrundi huyo ndipo alipopewa jukumu la kuinoa timu hiyo akitarajiwa kufanya makubwa.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, alitimuliwa kazi miezi miwili baadaye, huku klabu ikisema kuwa walifikia makubaliano ya kuvunja mkataba kwa maslahi ya pande zote, baada ya kushindwa kufikia makubaliano waliyowekeana. Ni kwamba Geita Gold ilikuwa haifanyi vizuri kwenye mechi zake za Ligi Kuu.

**HARUNA HERERIMANA - MBEYA KWANZA**

Hivi karibuni, klabu ya Mbeya Kwanza ilimtimua kocha wake Haruna Hererimana kwa madai ya timu kupata matokeo mabovu kwenye mechi za Ligi Kuu, ikimchukua kocha wa zamani wa Mbeya City, Maka Mwalwisi.

Hererimana, raia wa Burundi aliyewahi kuzifundisha klabu za Lipuli na KMC, alichukua jukumu la kuifundisha timu hiyo Agosti mwaka huu ikiwa inajiandaa kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza tangu ilipopanda. Mwanzoni alifanya vema, lakini ilipoanza kufanya vibaya tu, viongozi hawakuwa na muda wa kusubiri.

**GEORGE LWANDAMINA - AZAM FC**

Kocha huyu mkongwe raia wa Zambia, alitimuliwa katikati ya Desemba baada ya shinikizo kubwa kutoka kwa mashabiki wa Azam FC.

Lwandamina, kocha wa zamani wa Yanga, alipewa kibarua hicho Desemba mwanzoni mwaka jana na kuwa mmoja kati ya makocha waliopata fursa ya kufanya usajili wa kikosi chake cha msimu huu.

Lakini baada ya kuona kila kukicha afadhali ya jana, uongozi wa Azam ukaamua akae pembeni, na ikatangazwa kuwa ameandika barua ya kujiuzulu.

**JAMES OMOG - MTIBWA SUGAR**

Hakupishana siku nyingi na Lwandamina, naye alitimuliwa katikati ya Desemba baada ya jahazi la Mtibwa Sugar kuonekana kuzama siku hadi siku. James Omog, raia wa Cameroon, kocha wa zamani wa Azam FC na Simba, aliletwa nchini ikionekana kama itakuwa suluhisho la kuboronga kwa Mtibwa Sugar msimu uliopita, lakini ikawa afadhali hata ya msimu huo kuliko huu.

**HEMED MOROCCO - NAMUNGO**


Baada ya misimu miwili ya mafanikio, hatimaye Hemed Morocco naye ameondoka kwenye klabu ya Namungo.

Ilionekana mapema tu msimu huu kocha huyo Mtanzania kama hakuwa na maisha marefu, kwani viongozi wa Namungo alionekana kuja juu na kumpa mechi kadhaa ashinde la sivyo atafukuzwa. Kilichokuwa kinatokea ni kwamba anapopewa idadi ya mechi, anafanya vizuri.

Morocco ambaye aliifanya Namungo msimu uliopita kucheza hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, msimu huu umekuwa mgumu kwake kwenye Ligi Kuu.

Jumatano iliyopita baada ya kuchapwa nyumbani mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji, biashara ikawa imekwisha.

**JE, WAJUA?**



WINGA wa Chelsea, Hakim Ziyech hataitumikia Morocco kwenye michuano ya AFCON nchini Cameroon mwezi ujao kutokana na kocha wa timu hiyo ya taifa, Vahid Halilhodzic kutomjumuisha baada ya mapema Juni mwaka huu kukataa kuichezea katika mchezo dhidi ya Ghana akisingizia kuwa ni majeruhi licha ya timu ya matabibu kudai yupo fiti kucheza.







Mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Tunu Pinda, akimsikiliza bibi mjane baada ya kumkabidhi zawadi kwa ajili ya sikukuu ya Krismasi kwenye ibada iliyofanyika katika kanisa la Upendo Revival Christian Center TAG Area D jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mama Pinda awataka wajane kutojiona wanyonge

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKE wa Waziri Mkuu mstaafu, Tunu Pinda, amewataka wajane kutokata tamaa ya maisha na kujiona wanyonge pale wanapoondokewa na wenza wao na kuwaasa wajitume kufanya kazi kwa bidii ili kujipatia kipato kwa ajili ya mahitaji yao.

Akizungumza na wajane hao wakati wa chakula cha pamoja kilichoandaliwa na kanisa la Upendo Revival Christian Center TAG, lililoko Area D jijini Dodoma, alisema wajane wajione kuwa ni sehemu ya watu wengine na wala wasiwe na huzuni.

Alisema kitendo walichofanyiwa na kanisa hilo ni kuonyesha wao pia ni sehemu ya jamii ambayo inahitaji kusherehekea kwa pamoja na Watanzania wote.

"Kwangu mimi leo nimejifunza jambo kubwa sana hapa kanisani limeonyesha upendo wa hali ya juu sana kwa kuweza kukusanya idadi ya watu zaidi ya 400 na kula nao chakula.

"Natamani hata mimi kufanya jambo kama hili kwani ni upendo wa aina yake napenda kusema kuwa hili ni tukio kubwa na la kuigwa na watu wote," alisema.

Alisema pamoja na kanisa kuhubiri neno la Mungu pia wameweza kuwajali watu kiroho na kimwili kwa kushiriki nao chakula kwa pamoja na kuwapatia mahitaji mbalimbali kwa ajili ya kuwafariji badala ya kukaa kinyonge.

Mchungaji kiongozi wa kanisa hilo, Dk. Vangast Salumu, alisema kuwa ili nchi iweze kuwa na amani ni lazima haki itendeke.

Dk. Salumu akizungumza na waandishi wa habari kwenye ibada ya maalumu ya kumbukizi ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo iliyoambatana na utoaji wa sadaka kwa watoto wa mitaani, yatima, wajane na waishio katika mazingira mugumu.

Alisema katika kuelekea mwaka mpya wa 2022 kuna kila sababu ya kulinda na kutunza amani ya nchi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha amani inatendeka.

Mchungaji huyo alisema ili kuwa na taifa bora ni lazima kuwa na hofu ya Mungu pamoja na kuhakikisha haki inatendeka kwa kila mtu kulingana na alichokifanya.

"Nataka kusema kuwa tunaelekea katika mwaka mpya ujao ambao ni mwaka wa kubarikiwa ni lazima kulinda amani ya nchi sambamba na viongozi wa ngazi zote kutenda haki bila kuwa na ubaguzi wa aina yoyote.

"Ili nchi iweze kuwa na maendeleo lazima watu wawe na hofu ya Mungu, haki itendeke na ikitendeka inazaa amani," alisema.

Alisema kuwa kama hakuna haki amani haiwezi kuwapo pia ni muhimu kuwa na desturi ya watu kukaa meza moja na kuzungumza pale panapokuwapo dalili za kutofautiana kwa njia yoyote ile.

Katika hatua nyingine aliwataka Watanzania kufanya kazi kwa bidii na kuepukana na masuala ya kukaa vijiweni kwa kujadili mambo ambayo hayawasaidii kwa jambo lolote.

"Bila kufanya kazi kwa bidii na kuipenda kazi unayoifanya kamwe huwezi kubarikiwa kwani hata maandiko matakatifu yanaeleza wazi kuwa Mungu atazibariki kazi za mikono yako na kwenda mbali zaidi kwa kueleza kuwa asiyefanya kazi na asile," alisema.

Kuhusu kusherehekea Sikukuu ya Krismasi, aliwataadharisha waendeshaji wa vyombo vya moto kuwa makini wawapo barabarani.

Pia aliwataka Watanzania kuachana na tabia ya kuendesha vyombo vya moto wakiwa wamelewa kwa kuwa kwa kufanya hivyo kunaweza kusababisha madhara ya makubwa ikiwamo kupoteza maisha ya watu.

Akizungumzia kuhusu UVIKO-19 aliwataka Watanzania kuendelea na maombi pamoja na kuchukua hatua zinazoelekezwa na wataalamu wa afya sambamba na kuondokana na hofu.

"Ili kuepuka na janga hili ni muhimu sana kuendelea na maombi pamoja na kuachana na hofu kwani hofu inaweza kusababisha kifo hivyo hakuna sababu ya kuwa na hofu juu ya ugonjwa huu," alisema.

## Wajiandaa msimu kilimo kwa kununua mbegu bora za alizeti

**Renatha Msungu,** DODOMA

ASILIMIA 75 ya mbegu bora za zao la alizeti zimeshanunuliwa na wakulima kwa ajili ya kujiandaa na msimu wa mvua zinazotarajia kunyesha msimu huu.

Mbegu hizo zimekuwa zikiuzwa kwa bei ya ruzuku ya Sh. 7,000 kwa kilo mbili na mpaka sasa asilimia 75 ya mbegu zimeshanunuliwa na wakulima.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Bahi, Abdalah Mdiliko, alisema wamejipanga kuhakikisha wakulima wanatumia mvua zinazotarajiwa kunyesha hivi karibuni kwa kupanda mazao yanayostawi katika maeneo yao yaliyotifuliwa. Alisema wakulima wameichangamkia mbegu ya alizeti iliyotolewa na serikali kwa bei ya ruzuku hali inayomaanisha kutakuwa na ongezeko kubwa la uzalishaji wa zao hilo.

Alisema Wilaya ya Bahi ilipokea tani 28 za mbegu za alizeti na kila kata ilipatiwa tani moja kwa ajili ya kuwauzia wakulima.

Mdiliko alisema sasa mvua zimekaribia kuanza na wakulima wameanza kuandaa mashamba na wengine tayari wamelima wakisubiri mvua zinyeshe wapande.

Alisema wanasisitiza wakulima, kutifua mashamba kwa kuwa inasaidia maji yasitembee shambani na kwenda kusababisha mapormoko, watu wengi hawalimi mpaka chini wanalima kwa kuparua mvua inaponyesha maji yanapita na kuacha udongo ukiwa mkavu.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kijiji cha Kigwe, Jeremiah Sobayii, alisema wanaishukuru serikali kwa kutoa mbegu za ruzuku za alizeti ambalo ni zao la kimkakati hali itakayowezesha watu wa kipato cha chini kumudu bei.

Alisema kata hiyo yenye wakazi 3,900 shughuli kubwa ni kilimo na ufugaji.

# Waomba matuta barabarani kupunguza ajali

**Na Peter Mkwavila, C**HAMWINO

WAKAZI wa vijiji vya Buigiri, Chinangali na Mwegamile wilayani Chamwino, vilivyoko barabara kuu ya Dodoma-Morogoro, wameiomba serikali kuweka matuta na alama za barabarani kwenye maeneo hayo ili kupunguza vifo vinavyotokana na ajali za mara kwa mara.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti kwenye vijiji hivyo, walisema kuwa kutokana na watu kugongwa kama wanyama wanaiomba serikali kuweka matuta hayo barabarani ili kupunguza vifo ambavyo vinavyoleta hofu kwa wakazi wa maeneo hayo.

Godfrey Sinzila, alisema wanalazimika kuiomba serikali kuchukua hatua hiyo ya tahadhari ya kuwekewa matuta kwa kuwa wakazi hao wamejikuta wakigongwa mara kwa mara kutokana na magari yanayopita kutembea kwa mwendo kasi bila kujali kama kuna watu wanaotumia pia barabara hiyo.

"Tunamwomba Rais wetu msikivu wa wananchi Mama Samia Suluhu Hassan kutuangalia kwa jicho la huruma maana hivi sasa wakazi wa eneo hilo wanagongwa kama wanyama wa porini kutokana na madereva kutozingatia sheria za barabarani pamoja na kuwa maeneo hayo yana watu na wao wanatakiwa kuendesha kwa mwendo wa pole," alisema.

Naye Elizabent Mahunza, mkazi wa kijiji cha Chinangali alisema kuwa njia pekee ya kutoinyoshea serikali vidole ni kuwatatulia tatizo hilo la muda mrefu wanalolilia la kuwekewa matuta kwenye kipande hicho cha barabara kati ya Buigiri, Chinangali hadi Mwegamile.

Alisema kuwa wakazi wa maeneo hayo hawana imani na madereva wanaoendesha magari kutokana na uendeshaji wao wa kutojali watu hata na mifugo, suala ambalo limekuwa likisababisha kutokea vifo vya mara kwa mara.

Joram Mwaluko, alisema pamoja na kuomba matuta pia serikali waangalie uwezekano wa kupanua barabara hiyo ambayo imekuwa ikitumiwa na magari makubwa.

Awali, wakizungumza na waandishi wa habari wenyeviti wa serikali za vijiji hivyo, walisema kuwa serikali inatakiwa kuwanusuru wananchi wao kwa kuwawekea alama zitakazowezesha kuepuka ajali zinazotokea kwenye maeneo yao.

Yuda Ndalu, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Chinangali na Robert Chilewa, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Buigiri, walisema kuwa wananchi wao wamekuwa wakigogwa na kusababisha vifo na wengine kupata ulemavu wa kudumu.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chamwino, Keneth Yindi, akizungumza na waandishi wa habari, alikiri kupokea malalamiko hayo.

Yindi alisema kuwa wananchi hao wamechoshwa na madereva wanaopita kwa mwendo kasi kwenye barabara hiyo maana walio wengi wanasababisha ajali kwa kuwagonga watu kama wanyama.





## Wanne washikiliwa kwa tuhuma za uhalifu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia vijana watatu na mzee mmoja kwa tuhuma za kuvunja nyumba za watu usiku na mchana na kuiba mali mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema watuhumiwa hao pamoja na wa matukio mengine walikamatwa kufuatia msako maalumu uliofanyika kabla ya Sikukuu ya Krismasi.

Aliwataja vijana waliokamatwa kuwa ni William Sanga (25), mkazi wa Tukuyu wilayani Rungwe, Stamili Hemed (25) na Samson Kyando (27), wote wakazi wa Mikoroshini wilayani Rungwe pamoja na Mzee Freison Mbilinyi (52), mkazi wa Wilaya ya Kyela.

Kamanda Matei alisema katika upekuzi uliofanyika kwenye makazi ya watuhumiwa walikutwa na vitu mbalimbali zikiwamo redio na televisheni zenye ukubwa tofauti ambazo ni za wizi.

"Baada ya kuhojiwa William Sanga, alikiri kuiba mali hizo wilayani Rungwe na kwenda kuziuza wilayani Kyela kwa kushirikiana na watuhumiwa wengine, tunaendelea na upelelezi na ukishakamilika watafikishwa mahakamani," alisema Kamanda Matei.

Katika hatua nyingine Kamanda Matei, alisema jeshi hilo linamshikilia mtu mmoja raia wa Ethiopia kwa kuingia nchini bila kuwa na vibali vya jambo ambalo ni kinyume na sheria za uhamiaji.

Kamanda Matei alimtaja mtuhumiwa huyo kuwa ni Baraka Tadesa (19) na kwamba alikamatwa Desemba 23, mwaka huu saa 4:00 usiku katika kizuizi cha barabarani kilichoko Kayuki wilayani Rungwe, akiwa anasafiri kuelekea Malawi.

Alisema mtuhumiwa alikuwa anasafiri kwa kutumia gari lenye namba za usajili T933 CJC Toyota Carina ambalo lilikuwa linaendeshwa na dereva ambaye mpaka sasa hajafahamika kutokana na kutelekeza gari hilo na kutokomea kusikojulikana.

Kamanda Matei alisema jeshi hilo linaendelea na msako wa kumtafuta dereva huyo ili achukuliwe hatua za kisheria na kwamba mhamiaji haramu huyo anaendelea kushikiliwa ili kuchukuliwa hatua ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Alisema mtuhumiwa alikuwa akisafiri kutoka Kenya kuelekea Afrika Kusini kwa kupitia njia ya Malawi, aliwatahadharisha madereva kuacha kuwabeba wahamiaji hao kwa kuwa ni kinyume cha sheria za nchi.

# Watahadharishwa kula nyama isiyopimwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKATI Watanzania wakiungana na wenzao duniani kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka, wakazi wa Mkoa wa Mbeya wameshauriwa kutumia nyama iliyopimwa na wataalamu ili kuepuka kuhatarisha maisha yao kwa kula kitoweo kisicho salama.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na wataalamu wa nyama kutoka katika Bodi ya Nyama Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakati walipofanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka ya kuuza nyama jijini Mbeya kwa lengo la kujiridhisha na aina ya kitoweo kinachouzwa.

Ofisa wa Bodi hiyo, Mpoki Alinanuswe, alisema endapo wananchi watakula nyama ambayo haijapimwa wanaweza wakakumbwa na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kuharisha endapo kitoweo hicho kitakuwa si salama.

Alisema katika msimu wa sikukuu kama huu baadhi ya wananchi wamekuwa wakijinunulia wanyama na kuchinja wenyewe kwa ajili ya familia zao bila kuzingatia taratibu za uandaaji wa kitoweo hicho jambo ambalo alisema ni hatari.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wananunua nyama ambayo imechinjwa kwa kufuata taratibu za ukaguzi ikiwamo kwenye maduka ambayo yamethibitishwa kuwa yana ubora wa uuzaji wa nyama.

"Tunawataka wananchi wetu wazingatie sheria, hatupendi haya mambo yatokee ndiyo maana tunafanya huu ukaguzi, wananchi wanaweza wakakumbwa na magonjwa ya mlipuko endapo watakula nyama ambayo haijaandaliwa kwa kufuata taratibu," alisema Alinanuswe.

Aliwataka wafanyabiashara wa nyama kufanya biashara hiyo kwa kuzingatia sheria ili kuepuka kukumbwa na mkono wa sheria za usimamizi wa nyama.

Akizungumzia matokeo ya ukaguzi huo, Ofisa Mifugo wa Mkoa wa Mbeya, Samora Mshana, alisema walibaini baadhi ya maduka ya kuuza nyama kutokidhi vigezo na wakawapa muda wamiliki kufanya marekebisho.

Alisema mbali na hatua hizo pia walitoa elimu kwa wamiliki wa maduka hayo kuhusu taratibu za uuzaji wa nyama ili kuepuka kusababisha madhara kwa wananchi wanaotumia kitoweo hicho.

Alisema kwa mujibu wa sheria mfanyabiashara wa nyama ni lazima asajiliwe, eneo lake likaguliwe na kupewa kibali cha kufanya biashara hiyo, lakini baadhi huwa wanajisahau wakati wakiendelea kufanya biashara hali ambayo inawalazimu kufanya ukaguzi.

"Baadhi ya maduka kwa kiasi kikubwa yanafuata taratibu za uuzaji wa nyama, lakini machache ambayo tumeona hayako sawa tumetoa muda wa kufanyia marekebisho na kwa sababu ndiyo kazi yetu tutapita tena ili kujiridhisha," alisema Mshana.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi jijini Mbeya walilalamikia ongezeko la bei ya nyama katika kipindi hiki cha sikukuu wakisema imepanda kiasi kwamba baadhi wanashindwa kumudu kununua.

Mmoja wa wananchi hao, Shida Bakari, alisema wanaendelea kununua nyama liche ya bei hiyo kuwa juu kutokana na kwamba kwa sasa wanafahamu kila kitu kimepanda bei.

Nao baadhi ya wauzaji wa maduka ya nyama walisema kwa sasa wanauza nyama kulingana na pesa ya mteja tofauti na awali na walikuwa wanauza kwa kipimo cha kilo moja, nusu na robo.

Mgeni Ramadhani, ambaye ni mmoja wa wafanyabiashara hao alisema kwa sasa wanatumia mizani ya kidijitali kuuza nyama na hawahangaiki sana kama ilivyokuwa mwanzo.



Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Dk. Yahya Msuya, akijaribu kufungua maji kwenye miundombinu iliyowekwa na Shirika la SAWA chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), katika Zahanati ya Kijiji cha Shisyete Kata ya Shizuvi wilayani humo hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waumini wa Kikristo watakiwa kuomba mvua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAUMINI wa dini ya Kikristo mkoani Mbeya, wameitumia ibada ya Krismasi kumwomba Mungu alete mvua ili kuwezesha shughuli za kiuchumi kuendelea ikiwamo kilimo huku wakisema mwaka huu ni wa tofauti.

Waumini wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), Jerusalem Tempo lililoko Sokomatola jijini Mbeya walifanya ibaada maalumu juzi ya kuombe mvua wakidai kuwa kwa sasa shughuli za kilimo zimekwama kutokana na mvua kuchelewa.

Mchungaji wa kanisa hilo, Dk. Hudson Mwaijunga, alisema kwa sasa kuna mabadiliko makubwa ya tabianchi ambayo yanalikumba taifa na kwamba Wakristo wanatakiwa kuungana kuombea hali hiyo iondoke haraka. Alisema kulingana na taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA), inaonyesha kuwa tatizo hilo si kwa Mkoa wa Mbeya pekee bali ni kwa nchi nzima na kuna hatari ya wakulima kushindwa kulima.

Alisema baadhi ya maeneo ambayo wananchi walikuwa tayari wameshapanda mazao yanaweza yakakauka kutokana na kukosa mvua na kwa yale maeneo ambayo bado hawajapanda wanaweza wakashindwa kuendana na msimu.

"Tunaishukuru serikali kwa kuturuhusu kuendelea kufanya ibada pamoja na uwepo wa tishio la ugonjwa wa corona, sasa sisi tunatakiwa tuutumie muda huu kumwomba Mungu ili atushushie neema ya mvua maana tunaamini yeye ndiye anayeleta vyote," alisema Dk. Mwaijungu.

Hata hivyo, aliwataka Wakristo kuendelea kuzingatia taratibu zote zinazoelekezwa na wataalamu ili kujikinga na janga la corona ambalo kwa sasa linatishia duniani kote.

Baadhi ya waumini wa kanisa hilo walisema si jambo la kawaida kusherehekea Krismasi bila mvua kunyesha huku wakisema kipindi kama hiki miaka mingine wanakuwa wanapalilia mahindi.

Mmoja wa waumini hao, Ibrahim Malogoi, alisema pamoja na hali hiyo, lakini watahakikisha wanapambana kumwomba Mungu na wanaamini kwamba ataleta neema ya mvua. Alisema mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ni nyanda za kilimo na mvua isiponyesha kuna hatari kukawa na tatizo la njaa mwakani, akasema wataendelea kumwomba Mungu alete mvua hiyo ili wakulima waingie shambani.

"Tunaamini kwa maombi haya mvua itanyesha, tutakuwa na msimu wa kupanda na pia tutakuwa na msimu wa kuvuna mazao yetu, sisi wakristo tunaamini katika maombi na watu wengine wana imani zao hivyo tunaomba tuungane kila mtu na imani yake," alisema Malogoi.

Naye Veronica Mchome, alisema mwaka jana kipindi kama hiki mazao yalikuwa tayari yameota, lakini mwaka huu ni wa tofauti na umeambatana na vitu vingi visivyokuwa vya kawaida ikiwamo kupaa kwa bei ya pembejeo.





Baadhi ya watalii wakiogelea katika ufukwe wa kisiwa cha Kwale Unguja, kisiwa hicho ni miongoni mwa 10 ambavyo serikali imevikodisha kwa wawekezaji kwa ajili ya utalii. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kiwanda cha Sukari Z'bar chakabiliwa ukata

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HALI ya kifedha ya Kiwanda cha Sukari Zanzibar imeelezwa kuwa ni mbaya kutokana na kutokua na ardhi ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha miwa.

Meneja Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mahonda, Freak Rubeit Mtui, alitoa taarifa hiyo katika kikao cha pamoja cha majadiliano kuhusu changamoto hiyo kilichowahusisha baadhi ya mawaziri wa Serikali ya Zanzibar na watendaji wa kiwanda hicho.

Katika kikao hicho kilifanyika jana kiwandani hapo Mahonda, Meneja huyo alisema uzalishaji wa sukari umesita kutokana na kiwango kidogo cha miwa kilikosabishwa na kutokuwa na ardhi ya kutosha kwa ajili ya kilimo hicho.

Alisema kiwanda kinakabiliwa na changamoto ya ardhi kwa ajili ya uzalishaji wa miwa ili kuzalisha sukari inavyotakiwa.

Alisema kuwa wakati wanasaini mkataba na serikali kwa ajili ya uendeshaji wa kiwanda hicho mwaka 2010 walipaswa kuwa na hekari 6,644 na kwa sasa wana upungufu wa hekari 2,700.

Meneja Freak alisema matarajio ya kiwanda ni kuwa na hekari 6,644 sambamba na kuongeza wakulima wadogo ili kufikia hekari 10,000.

Alisema mpaka sasa wana wakulima wadogo 317 na vikosi vya serikali vinavyoshirikiana na kiwanda hicho kwa ujumla wana hekari zaidi ya 900 ambazo wanalima wakulima wadogo wa miwa.

Alisema kiwanda kinafanya kazi kwa asilimia 30 na hakijafikia lengo la uwezo wake wa uzalishaji, kwa msimu wa mwaka huu unaoishia 2021 wamezalisha tani 7,000 za sukari tofauti na uwezo wa kiwanda kuzalisha tani 22,000 kwa mwaka.

Alisema anaamini serikali italiangalia jambo hilo la upatikanaji wa ardhi na kuongeza uzalishaji wa miwa kwa wakulima wadogo ili kiwanda kiweze kufikia malengo yao ya kuona sukari wanayozalisha inatosheleza katika soko la Zanzibar.

Alisema kikifanya kazi ipasavyo kina uwezo wa kuzalisha umeme megawati 10 ambazo nane zitatolewa na kuingizwa katika gredi ya taifa na spirit kwa ajili ya hospitali, nishati ya kupikia na mahitaji mengine mbalimbali.

Waziri wa Ardhi, Riziki Pembe, alisema lazima kuwe na ushirikiano na kuwahamasisha wananchi kulima kilimo cha miwa ili kukipa uwezo kiwanda kuzalisha sukari.

Akizungumzia maeneo yanayotumiwa na vikosi vya SMZ na wananchi kwa ajili ya kilimo kingine alisema lengo sio kuwanyang'anya maeneo hayo bali ni kuona wanalima miwa na kuuza kwa kiwanda ili waweze kupata malighafi hayo na kuongeza uzalishaji wa sukari.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, alisema lengo la kikao hicho ni kujadili changamoto zinazokikabili kiwanda hicho hasa katika sekta ya uzalishaji wa sukari, kujiendesha kibiashara na kuongeza kipato.

Alisema ili kufikia lengo hilo ni lazima kiwanda kipate malighafi ya miwa ambayo ni muhimu katika uzalishaji wa sukari na wananchi kupata ajira.

Mudrik Ramadhan Soraga Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, alisema jukumu lao ni kukuza uwekezaji na kuwavutia wawekezaji na kwamba wanalichukua suala kwa uzito wa kipekee, kufanikiwa kwa kiwanda hicho ni chachu ya kuvutia viwanda vingine.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema serikali imeamua kubinafsisha kiwanda hicho ikiwa na lengo la kuona Zanzibar inajitosheleza kwa sukari hiyo na kupunguza kiwango cha kuagiza nje ya nchi.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Dk. Soud Nahoda Hassan, alisema lengo lao ni kuona kiwanda hicho kinajiendesha katika uzalishaji wa sukari kwa kiwango kinachohitajika kwa kupata maeneo ambayo yatawasaidia katika uzalishaji wa miwa.

Alisema changamoto ya kiwanda hicho sasa ni fursa kwa kuona maeneo yanapatikana kwa ajili ya ulimaji wa miwa na kukiwezesha kiwanda hicho kupata miwa ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa sukari.

# Wanne wafariki dunia kwa kula samaki mwenye sumu

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WATU wanne wamefariki dunia na wengine zaidi ya 30 wamedhurika kutokana na kula samaki aina ya kasa anayesadikiwa kuwa na sumu huko Mtemwe, Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kutokana na vifo hivyo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametuma salamu za rambirambi kwa familia za marehemu.

Katika salamu hizo Dk. Mwinyi ameeleza kusikitishwa na vifo hivyo na kuzinasihi familia za marehemu hao kuwa na subira na ustahamilivu katika kipindi hiki kigumu cha msiba pamoja na kumwomba Mwenyezi Mungu kuwaponya kwa haraka waliodhurika baada ya kula samaki huyo.

Rais Dk. Mwinyi katika salamu hizo, alisema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara yake husika itaendelea kuhakikisha wote waliodhurika wanaendelea kupatiwa tiba ili waweze kurudi katika hali zao kawaida kiafya.

Tukio hilo limetokea juzi na watu hao wapo katika Hospitali ya Kivunge Mkoa wa Kusini Unguja wakiendelea kupatiwa matibabu.

Akiwatembelea majeruhi hao Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A Unguja, Sadifa Juma, aliwataka wananchi kuacha kula samaki ya aina hiyo bila kuchunguzwa kama ni salama.

# JUMAZA yaipongeza serikali kuchagua kampuni uingizaji vileo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) imempongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum Masoud Mohamed Ali kwa kuzitaja kampuni tatu zitakazopewa kibali cha kuingiza vileo mwaka wa fedha 2021/2022.

Pongezi hizo zimetolewa na Katibu wa Jumuiya hiyo, Shekhe Ali Abdalla Amour, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Vuga kuhusu tamko la waziri la kusimamia sheria ili kuepusha migogoro inayojitokeza katika biashara hiyo.

"Kwa dhati tunampongeza waziri kwa ahadi na tamko lake kusimamia sheria kwa sababu kuna kampuni hazina sifa bado zimekuwa zikifanya biashara ya kuingiza vileo na kampuni ambazo kazi yake ni kutegeneza majiko, cha ajabu zinafanya biashara ya vileo," alisema Shekhe Amour.

Alisema hatua hiyo itasadia kuepusha vitendo vya uvunjaji wa sheria ambavyo vimekuwa vikijitokeza katika utoaji wa leseni za baa pamoja na vibali vya uingizaji wa vileo.

Alisema kifungu cha 33 (1) kimesema kibali cha kuingiza vileo kitatolewa kwa waingizaji wasiozidi watatu na kuzingatia vigezo ambavyo ni lazima muagizaji awe Mzanzibar, mlipakodi awe na ghala pamoja na gari ya kusambazia vinywaji.

Aidha, alisema kifungu cha 28 (k) kimeweka masharti kabla ya kutolewa leseni ya baa lazima iwe umbali wa mita 1000 kutoka katika maeneo ya huduma za jamii kama nyumba za ibada, shule, hospitali na makazi ya watu.

Hata hivyo, alisema mwaka wa fedha 2020/2021 leseni za baa na vibali vya uingizaji vileo zilitolewa kinyume na Sheria ya Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar (ZLB) hali iliyosababisha kuzuka bugudha katika jamii na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Awali, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, Masoud Ali Mohamed alisema Bodi ya Vileo inakusudia kufanya uhakiki wa kina kabla ya kuanza utoaji wa vibali vya uingizaji vileo pamoja na leseni za baa. Alisema pia uhakiki huo utafanyika katika hoteli za kitalii ambazo zimekuwa zikidaiwa kuingiza vileo kinyume na sheria na kuikosesha mapato serikali.

Alisema vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kusimamia sheria ya vileo kwa umakini hasa katika maeneo ya bandari na uwanja wa ndege ili kudhibiti biashara hiyo kinyume na sheria.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar, Khamis Haji, alisema kabla ya kufungua zabuni ya vibali vya uingizaji vileo kampuni zote ambazo zitajitokeza lazima italazimika zikaguliwe ili wamiliki wake waionekane kama wana sifa ya Mzanzibar.

Pia alisema Bodi haitasita kuchukua hatua za kisheria kwa kampuni yoyote itakayobainika kufanya biashara ya kuingiza na kusambaza vileo kinyume na sheria namba 9 ya mwaka 2020.

Kiongozi Mwandamizi wa Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Shida Kombo, alisema wameanza kufanya uchunguzi dhidi ya kampuni zinazomilikiwa na wageni na kufanya biashara ya uingizaji vileo wakati ni kinyume na sheria.

# SHAMRASHAMRA ZA SIKUKUU



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakisherehekea sikukuu ya Boxing Day katika fukwe ya Coco Oysterbay, jijini humo jana. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**









HABARI KIMATAIFA

# Viongozi duniani wamlilia Askofu Tutu

## • Boris Johnson ataja mchango wake Afrika Kusini



Askofu Desmond Tutu akiwa pamoja na Nelson Mandela. **PICHA ZOTE : MTANDAO**

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

ASKOFU Desmond Tutu wa Afrika Kusini, ambaye ni mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel, ameaga dunia akiwa na miaka 90.

Askofu Tutu, mshindi wa tuzo hiyo mwaka 1984, amefariki jana, kwa mujibu wa vyombo vya habari kimataifa, atakumbukwa kwa kusaidia Afrika Kusini kumaliza ubaguzi wa rangi.

Aligunduliwa kuugua saratani ya kibofu, mwishoni mwa miaka ya 1990 na katika miaka ya hivi karibuni alilazwa hospitalini mara kadhaa kutibiwa magonjwa yanayohusiana na matibabu yake ya saratani.

Juni 10, mwaka huu, Desmond Tutu ambaye alitimiza umri wa miaka 90, tabia yake ilikuwa ni kuzungumza mara chache sana hadharani.

Rais Cyril Ramaphosa, amesema kwamba kifo cha muhudumu huyo wa kanisa kimeadhimisha kwa mara nyingine msiba ya kizazi muhimu cha taifa hilo.

"Desmond Tutu alikuwa mzalendo asiye na kifani. Kufariki kwa Askofu Mkuu Emeritus Desmond Tutu ni msiba katika kuaga taifa letu kwenye kizazi cha watu mashuhuri wa Afrika Kusini, ambao wametuachia urithi wa Afrika Kusini iliyokombolewa," Rais Ramaphos, alisema.

Alisema kwamba Askofu Tutu, alisaidia katika kurithi taifa la Afrika Kusini lililokombolewa.

Askofu Tutu alikuwa mmoja ya viongozi maarufu Afrika Kusini na ugenini.

Alifariki dunia kwa amani katika Kituo cha Utunzaji cha Oasis huko Cape Town asubuhi ya jana, alisema Dk. Ramphela Mamphele, Kaimu Mwenyekiti wa Askofu Mkuu Desmond Tutu IP Trust na Mratibu wa Ofisi ya Askofu Mkuu, katika taarifa kwa niaba ya familia ya Tutu.

Tutu alionekana kuwa na sura dhaifu Oktoba, mwaka huu, huku akibebwa akiwa kwenye parokia yake ya zamani katika Kanisa Kuu la St George's mjini Cape Town, ambayo lilikuwa kimbilio salama kwa wanaharakati wa kupinga ubaguzi wa rangi, kwa ibada ya kuadhimisha miaka 90 ya kuzaliwa kwake.

Alitunukiwa tuzo ya Nobel mwaka 1984 kwa jukumu lake katika mapambano ya kukomesha mfumo wa ubaguzi wa rangi.

Kifo cha Tutu, kinajiri wiki chache tu baada ya Rais wa mwisho wa enzi za ubaguzi wa rangi, FW de Clerk, kufariki akiwa na umri wa miaka 85.

Rais Ramaphosa, alisema kwamba Tutu alikuwa kiongozi maarufu wa dini, mwanaharakati dhidi ya ubaguzi wa rangi na mpiganiaji wa haki za binadamu kote duniani.

Alimwelezea kuwa mtu mzalendo, kiongozi mwenye misimamo aliyetoa maana kwa ufahamu wa Biblia kwamba imani bila matendo ni sawa na kifo.

"Alikuwa mtu mwenye ufahamu wa ajabu, mwadilifu na asiyeweza kushindwa dhidi ya nguvu za ubaguzi wa rangi, pia alikuwa mpole na mwenye huruma kwa wale ambao walikuwa wamepitia dhuluma na vurugu chini ya ubaguzi wa rangi, mbali na watu waliokandamizwa kote ulimwenguni."

**Inasikitisha, lakini alikuwa mzee na aliitumikia nchi yake vizuri sana na ni msiba mzito sana wakati huu ambapo kuna mgogoro wa kiongozi nchini na duniani.**



Alitawazwa kama padre mwaka wa 1960 na kuhudumu kama askofu wa Lesotho kuanzia 1976 hadi 1978, askofu msaidizi wa Johannesburg na mkuu wa parokia ya Soweto.

Alikuwa Askofu wa Johannesburg mwaka 1985, na akateuliwa kuwa Askofu Mkuu wa kwanza mweusi wa Cape Town.

Alitumia nafasi yake ya hadhi ya juu kuzungumzia ukandamizaji dhidi ya watu weusi nchini mwake, siku zote akisema nia yake ni ya kidini na si ya kisiasa.

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Andrew Harding anasema ni vigumu kuilezea Afrika Kusini bila kumtaja Askofu Tutu.

Anasema kwenye harakati za kupigania nchi hiyo, wengi waliishia kuuawa na wengine kufungwa gerezani.

Anasema askofu huyo wa kianglikana alikuwapo katika kila hatua, akifichua watu, akishikilia vuguvugu la ukombozi kuwajibika na kusababisha serikali za magharibi kufanya zaidi kutenganisha serikali ya wazungu wachache.

Mchambuzi huyo anasema, demokrasia ilipowadia, Tutu alitumia mamlaka yake ya kimaadili kusimamia Tume ya Ukweli na Maridhiano, ambayo ilitaka kufichua uhalifu wa serikali ya wazungu wachache.

**VIONGOZI WAMLILIA**

Katika ibada ya Boxing Day huko Oasis Frail Care Centre mjini Cape Town, jana, kwenye kanisa la St George, Mchungaji Michael Weeder, alitoa heshima kwa Askofu Tutu, akisema "ilikuwa hatua ya kuadhimisha" kabla ya kuwataka waumini wachache wa parokia waliopo kanisani, kuinamisha vichwa vyao katika dakika moja kwa kukaa kimya.

"Inasikitisha, lakini alikuwa mzee na aliitumikia nchi yake vizuri sana na ni msiba mzito sana wakati huu ambapo kuna mgogoro wa kiongozi nchini na duniani," alisema Ntokozo Mjiyako, wakili mjini Cape Town.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Canterbury, Justin Welby alimsifu Askofu Tutu kama nabii na kuhani, huku bilionea wa Uingereza Richard Branson, akisema "ulimwengu umepoteza mtu".

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, alisema jukumu muhimu la Tutu lilikuwa katika mapambano ya kuunda Afrika Kusini mpya na Waziri Mkuu wa Norway, Jonas Gahr Stoere, alikumbuka "akimtaja kama mtu ambaye alionyesha nguvu ya upatanisho na msamaha".

"Sisi ni bora zaidi kwa sababu alikuwa hapa," Bernice King, binti wa Martin Luther King, alisema.

Ofisa wa Shirika la Ukombozi wa Palestina, Wasel Abu Youssef, alisema Tutu alikuwa mmoja wa wafuasi wakubwa wa Palestina.

Tutu na rafiki yake wa muda mrefu Mandela, waliwahi kuishi kwenye mtaa mmoja katika kitongoji cha Soweto, Afrika Kusini na hivyo kuufanya kuwa Mtaa wa Vilakazi, pekee duniani kuwa na washindi wawili wa Tuzo ya Amani ya Nobel, eneo moja. **BBC**

# MBEYA CITY SASA YASALIMU AMRI KWA SIMBA, YANGA

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAADA ya kushuka dimbani michezo tisa bila kupoteza, hatimaye timu ya Mbeya City imepoteza kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

**Mbeya City ilikuwa ni moja kati ya timu tatu ambazo hazijapoteza, ikiwamo timu za Simba na Yanga na imekuwa ya kwanza kati ya hizo tatu kudondosha pointi tatu katika mchezo mmoja.**

Ijumaa iliyopita, kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga, ilipokea kipigo cha mabao 3-2 na kuhitimisha rekodi yao nzuri, baada ya kucheza mechi tisa, ikishinda tatu, sare sita, kabla ya kupoteza kwenye mechi yake ya kumi.

Ilionekana kama Mbeya City ingeendelea na rekodi hiyo hadi raundi ya 10, lakini bao la mkwaju wa penalti dakika ya 90 lililofungwa na Abdul Selemani, lilifuta ndoto hizo.

"Tulicheza vizuri, ila haikuwa bahati yetu leo, nawapongeza sana wachezaji wangu walipambana, lakini siku ambayo haikuandikwa, basi hata ufanye nini huwezi kushinda," alisema Kocha Mkuu wa timu hiyo Mathias Lule.

Wakati Mbeya City ikipoteza, Simba na Yanga nazo zilikuwa zimeshacheza mechi tisa bila kupoteza, Yanga ilitarajia kucheza jana usiku dhidi ya Biashara United, huku Simba ikitarajiwa kushuka tena dimbani siku ya mwaka mpya, Jumamosi ijayo dhidi ya Azam FC zikiwa mechi zao za raundi ya 10 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo, Lule alisema ana imani wachezaji wake si wa kiwango kikubwa kama ilivyo kwa klabu kubwa hapa nchini, ila amefanikiwa kukaa nao na kuwafanya kuwa wakubwa.

Alisema aliwataka wachezaji wake kuangalia zaidi maisha yao ya soka ya mbele na kuwasisitizia kwamba kuonyesha kiwango bora ndani ya timu hiyo inamfungulia milango kwa timu kubwa.

"Niliwatolea mifano juu ya kipato wanachokipata na kuwajengea kisaikolojia, ubora watakaonyesha ndani ya Mbeya City itakuwa nafasi yao ya kwenda kucheza soka klabu kubwa hapa nchini au nje.

"Niliwaeleza wasiogopeshwe na majina makubwa ambayo tutaenda kucheza nao kwa sababu wote wanacheza mpira mmoja kwa kutumia miguu miwili, nikawaeleza kwamba wao watakuwa bora zaidi ya hao ambao wanazungumzwa," alisema Lule.

Alisema mambo hayo mawili ndiyo yamesaidia kuibadilisha Mbeya City kuwa tofauti na misimu mitatu iliyopita na hatimaye kuwa timu ambayo inazungumzwa kwa kufanya vizuri katika ligi.

**IKO HIVI...**



Kocha wa timu ya vijana wanaolelewa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), Maalim Saleh, akiwapa maelekezo vijana hao wakati wa mazoezi yaliyofanyika Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Netiboli Muungano yapigwa kalenda

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Muungano ya mchezo wa netiboli yaliyokuwa yafanyike kesho, Desemba 28 visiwani Zanzibar, yamesogezwa mbele hadi Januari 29, mwakani ili kupisha sherehe za Mapinduzi.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta), Devota Marwa (pichani chini), alisema mashindano hayo yatashirikisha timu sita kutoka Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar zitashiriki timu ambazo zimepanda daraja.

"Kwa sasa tumevunja kambi mpaka mwakani, kila timu inaendelea na mazoezi ili kujiweka sawa kuelekea michuano hiyo," alisema.

Alizitaja baadhi ya timu ambazo zitashiriki mashindano hayo kuwa ni Uhamiaji pamoja na timu ya Magereza.

Aidha, aliwataka wachezaji wasichoke kufanya mazoezi kwani tarehe ya mashindano iliyopangwa haipo mbali.

"Ninaomba wachezaji wasichoke kujinoa, tarehe haipo mbali wakikaa bila kufanya mazoezi viwango vyao vitapungua," alisema.



# Simbu, Failuna washindwa kutamba Karatu

**Mwandishi Wetu, Karatu**

WANARIADHA nyota wa mbio ndefu nchini, Failuna Abdi na Alphonce Simbu, wameshindwa kutamba kwenye mbio za kilomita tano na 10 katika Tamasha la Karatu lililofanyika kwa siku mbili kwenye viwanja vya Mazingira Bora mjini hapa.

Simbu alimaliza wa sita akitumia dakika 32:56:32 akiachwa kwa sekunde kadhaa na bingwa, Faraja Lazaro aliyekimbia kwa dakika 32:00:42 kwenye mbio za kilomita 10 za wanaume.

Failuna mshindi wa mwaka jana, msimu huu alimaliza wa saba akitumia dakika 20:30:03 akiachwa kwa zaidi ya dakika 1:30 na bingwa mpya wa mbio hizo, Natalia Elisante aliyetumia dakika 18:34:20 kwenye mbio za kilomita tano za wanawake.

Kwenye mzunguko wa kwanza, Failuna alikuwa akiongoza akiwa sanjari na Natalia, kabla ya kuanza kupitwa akiwa amebakiza kilomita 2 kumaliza mbio hizo na kumaliza wa saba.

Nyota wengine waliochuana kwenye mbio hizo zilizodhaminiwa na Olympic Solidariry (OS), kupitia Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC) ni Mayselina Mbua aliyemaliza wa pili akitumia dakika 18:51:28, Annastazia Dolomongo aliyetumia dakika 19:30:83 na kuwa watatu.

Wengine waliomfunika Failuna ni Asha Salum, Aisha Lubuma na Sarah Ramadhan.

Upande wa wanaume walichuana kwenye mbio za kilomita 10, nyota wa Tanzania wa mbio ndefu, Alphonce Simbu, alimaliza wa sita akitumia dakika 32:56:32 akiachwa kwa sekunde kadhaa na bingwa, Faraja Lazaro aliyekimbia kwa dakika 32:00:42.

Simbu alikiri kuzidiwa kwenye mzunguko wa mwisho na nyota wengine walioongozwa na Lazaro, Gabriel Geay na Fabian Sulle waliomaliza kwenye nafasi ya pili na ya tatu.

"Mimi ni mzoefu zaidi kwenye marathon, hii ya kilomita 10 ina wenyewe, ndio sababu vijana walinipita," alisema Simbu.

Geay anayeshikilia rekodi ya taifa ya marathon ya saa 2:04 alitumia dakika 32: 11:70 na Sulle alitumia dakika 32:18:35 kumaliza mbio ya Karatu, wengine waliompiku Simbu ni Shingade Giniki na Inyasi Sulle ambao walimaliza wa nne na tano.

Naibu Katibu Mkuu wa TOC, Suleiman Jabir, alisema kamati hiyo iliomba Olympic Solidarity iwadhamini kuandaa tamasha hilo mjini Karatu kutokana na historia ya michezo hasa riadha kwenye wilaya hiyo ambayo amezaliwa nyota aliyewahi kuvunja rekodi mbili za dunia za mita 1500 na maili moja kwa nyakati tofauti, Filbert Bayi.

"Washiriki wote wanagharamiwa chakula na malazi na TOC, lakini pia tunatoa vifaa kwa baadhi ya wachezaji na zawadi kwa washindi," alisema Jabir.

## ZISIKUPITE

### NYOTA KUBAKISHWA

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe, amesema hatawaachia wachezaji wake, Dwight Gayle, 32 na kiungo wa kimataifa wa Ireland, Jeff Hendrick, 29. ***(Chronicle)***

### CABALLERO MKATABA MPYA

KLABU ya Southampton inaangalia uwezekano wa kuongeza mkataba na golikipa wa zamani wa Argentina, Willy Caballero, 40. Kipa huyo alisaini mkataba utakaomweka hapo hadi Januari 5. ***(Mail)***

### AGOMBEWA NA KLABU SITA

KLABU sita za Championship, Bournemouth, Fulham, Huddersfield Town, Nottingham Forest, Stoke City na West Brom - zinamwania straika wa Aston Villa, Keinan Davis, 23. ***(Football Insider)***

### TRIPPIER KWENYE RADA

NEWCASTLE inakabiliwa na ushindani kutoka Manchester United na Tottenham Hotspur katika kinyang'anyiro cha kuwania saini ya mlinzi wa England, Kieran Trippier, 31 kutoka klabu ya Atletico Madrid. ***(90min)***

### JOHNSTONE LULU EPL

TOTTENHAM, Newcastle, West Ham na Rangers wanagombania kumsajili mlinzi wa West Brom na England, Sam Johnstone, 28. ***(Teamtalk)***

### AUBAMEYANG KUONDOKA

ARSENAL ipo tayari kusikiliza ofa kwa ajili ya mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 32, baada ya kuvuliwa unahodha mwezi huu. ***(ESPN)***

### DIGNE KUTUMIA NAPOLI

NAPOLI wanaangalia uwezekano wa kumpa mkataba beki wa Everton na Ufaransa, Lucas Digne, 28, ambaye amedokeza kuwa anataka kuondoka pale Goodison Park Januari. ***(Foot Mercato)***

### NYOTA BARCA KUONDOKA

BARCELONA wanahangaika kumwachia mlinzi Mfaransa Samuel Umtiti, mwenye umri wa miaka 27, na mchezaji nyota wa Brazil, Philippe Coutinho, 29, kwa sababu wachezaji wote wawili hawataki kuacha mikataba yao minono pale Nou Camp. ***(TodoFichajes)***

### DELE KURUHISIWA KUONDOKA

TOTTENHAM Hotspur wanaangalia namna ya kuwaondoa kwende klabu hiyo mlinzi, Matt Doherty, 29, na kiungo wa kati wa England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 25. ***(The Athletic)***

### DIAZ KUCHUKUA NAFASI YA 4

LIVERPOOL wanawafuatilia kwa karibu winga wa Porto na Colombia, Luis Diaz mwenye, 24, kama mchezaji mbadala wa Sadio Mane, 30, ambaye anaelekea kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika ambapo atalichezea taifa lake la Senegal mwezi ujao. ***(FourFourTwo)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SAKA AAMUA KUJIFUNGA ARSENAL MIAKA 6 ZAIDI

●●● Mwanzoni alisaini kubaki hapo Emirates hadi msimu wa 2023-24, lakini sasa atakuwapo mpaka...

**LONDON,** England

ARSENAL wameripotiwa kuwa na matumaini ya kumsainisha Bukayo Saka mkataba mpya wa miaka sita hadi msimu wa majira ya joto wa mwaka 2027.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England anaendelea kuimarika chini ya kocha Mikel Arteta, akiwa amepata mabao manne na asisti nne katika mechi 20 za michuano yote msimu huu.

**Saka alisaini mkataba mpya na klabu hiyo mwaka jana, huku masharti yake ya sasa yakimbakiza hadi mwishoni mwa msimu wa mwaka 2023-24.**

Hata hivyo, mwanahabari Ekrem Konur anadai kwamba Arsenal sasa wamedhamiria kujihakikishia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 anasalia kwa muda mrefu zaidi, kwa ofa ya mkataba hadi 2027.

Mkataba kama huo ungemfanya Saka kusalia katika klabu hiyo baada ya kutimiza umri wa miaka 25.

Mshambuliaji huyo tayari ameshafunga mabao 15 na asisti 25 kwenye michezo 108 aliyoichezea klabu yake hiyo ya utotoni.

CHEZA USHINDE KASINO




# DE JONG KUTIMKA BARCA



**MADRID,** Hispania

MAISHA ya Luke de Jong pale Barcelona yanaonekana kufika mwisho na anajipanga kujiunga na klabu ya Cadiz ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Mshambuliaji huyo wa kati wa Uholanzi amebaki yeye tu kufanya maamuzi ili dili iweze kukamilika.

Mundo Deportivo limeripoti kwamba bosi wa Cadiz, Alvaro Cervera hatimaye anaweza kuipata saini ya De Jong kwani alikuwa akihitaji huduma ya mchezaji huyo kwa muda mrefu.

Tetesi za hivi majuzi zilidai kuwa Diego Costa atakuwa njiani kuelekea klabuni hapo, lakini inaonekana wamepata mtu wao.

De Jong alitua Barcelona kama mchezaji wa muda anayeweza kuwasaidia mwishoni mwa dirisha la usajili la majira ya joto.

Lakini kutokana na ujio wa kocha Xavi Hernandez, inaonekana wazi kuwa hayupo kwenye mipango yake, akiwa amecheza dakika nane pekee tangu Xavi achukue nafasi hiyo.

# 2021 mwaka mbaya kwa Ram



**PARIS,** Ufaransa

MWAKA 2021 umekuwa mgumu zaidi kwa mlinzi, Sergio Ramos na hatousahau tangu ulivyoanza hadi unavyoisha kwa mambo yaliyomtokea, Marca limeeleza.

Januari ilionekana kama kuwa na neema baada ya Real Madrid kuonyesha dalili za kumpa mkataba mpya na kwenda na timu ya taifa kwenye michuano ya Ulaya, lakini mambo ghafla yalibadilika na majanga yakaanza kumwandama.

Alipata tatizo la tumbo hali iliyosababisha kukosa mechi za Real Madrid na katikati ya mwezi huo alikumbwa na tatizo lingine la mguu katika mchezo waliopoteza katika michuano ya Supercopa de Espana. Februari tatizo lake la mguu lilihitaji kufanyiwa upasuaji na alifanyiwa, hali iliyosababisha kukaa nje ya dimba kwa wiki.

Machi aliaga kuichezea timu ya taifa wakati kampeni ya michezo ya kufuzu Kombe la Dunia ilipoanza baada ya Luiz Enrique kutokuwa na mipango naye.

Aprili Ramos hakucheza hata dakika moja kwa Madrid kwa mara ya kwanza tangu Mei mwaka 2013.

Mei alisafiri na kikosi cha
Real Madrid hadi Lon
kabili Chelsea amba
Blancos' walitolewa
michuano ya Ligi ya
wa Ulaya.

Juni ndiyo ilikuwa
wa Ramos kuwa seh
klabu ya Real Madrid
ma hakutaka kuondok

PSG walimsaini Ram
huku akitarajiwa kut
ansa akifuatiwa na
makubwa kutua klabu

Agosti, Septemba
toba, Ramos hakuwa
chezea Paris Saint-
wakati Novemba 9,
mazoezini, lakini ha
kucheza hadi tarehe 2
cheza dhidi ya Saint-
na baadaye alirejea
orodha ya majeruhi.

LIVE IN PLAY

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA



PAKUA SASA

# GGML yaidhamini Geita Gold FC kwa mil. 500/-



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Wayne Louw (kulia), akipeana mkono na Mwenyekiti wa Klabu ya Geita Gold, Leonard Bugomola, baada ya kusaini mkataba wa udhamini wenye thamani ya Sh. milioni 500 kati ya GGML na klabu hiyo, katika Halmashauri ya Mji wa Geita wiki iliyopita. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML), imeidhamini Klabu ya soka ya Geita Gold kwa mkataba mnono wa thamani ya Sh. milioni 500 kwa msimu wa 2021/22.

**Mkataba huo unaifanya GGML kuwa mdhamini mkuu wa Geita Gold FC wenye lengo la kuiwezesha klabu hiyo kushiriki kikamilifu katika Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu huu na shughuli nyingine za klabu hiyo.**

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, GGML inapata haki za kuwa mdhamini mkuu wa klabu katika mechi zote au tukio lolote linalohusiana na msimu wa Ligi Kuu ya NBC 2021/22.

Pia GGML inapata fursa ya kuwa mdhamini katika matukio yote yajayo ndani ya klabu kwa kuzingatia sheria na masharti maalum yaliyobainishwa katika makubaliano hayo na kwa mujibu wa Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii kwa 2021-2022.

Akizungumza wakati wa hafla ya kusaini makubaliano hayo katika ofisi za makao makuu ya Halmashauri ya Mji wa Geita zilizoko Magogo Geita mjini, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Wayne Louw, alisema kampuni yake imetia saini mkataba huo kwa sababu inaamini katika kusaidia na kushirikiana kwa manufaa ya pande zote mbili yaani kampuni na jamii inayowazunguka.

“Tumeona watu wa Geita wanapenda soka. Kwa hiyo, kama mshirika na mdau wa Geita, GGML imeamua kuisaidia timu hii ili kutimiza ndoto na malengo ya klabu kwa kuhakikisha inapata mahitaji yote muhimu. Ushindi na kupata kombe ni matokeo ya juhudi za pamoja za wachezaji, uongozi na wadau wote,” alisema.

Aliongeza kuwa fedha hizo za udhamini ambazo kampuni itatumia kusaidia klabu ni sehemu ya jumla ya bajeti ya Sh. bilioni 9.2, ambayo imetengwa kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Uwajibikaji kwa Jamii wa 2021.

Katika kipindi cha miaka mitatu, GGML imetumia zaidi ya Sh. bilioni 30 kusaidia maendeleo na ustawi wa jamii inayowazunguka katika nyanja mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Alisema GGML pia imefadhili ujenzi wa Uwanja wa Geita kwa thamani ya Sh. bilioni 1.9 na uwanja huo ukikamilika, utakuwa mkubwa na wa kisasa zaidi kwa mjini Geita.

“Miradi hii yote inatekelezwa kwa sababu kampuni inaona kuwa ni wajibu wa kimaadili kuhakikisha kwamba watu wanaoshiriki katika biashara yetu wanapata maisha bora kwa sisi kuwa hapa,” alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilson Shimo, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo alipongeza GGML kwa dhamira yake ya kuleta mapinduzi ya soka mkoani Geita.

“Nia ya GGML kufadhili timu yetu inaonyesha jinsi gani kampuni imekuwa karibu na jamii yetu.

“Pia nimeambiwa hapa kwamba GGML imeisaidia Geita Gold Football Club tani mbili za mchele na lita 100 za mafuta ya kupikia kama kifurushi cha Krismasi na mwisho wa mwaka. Nina hakika hilo litawapa motisha ya kushinda mchezo huo muhimu unaoendelea.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Zahara Michuzi, alieleza kuwa licha ya kuwa Halmashauri ya Mji wa Geita na wakazi wa Geita wanamiliki klabu ya Geita Gold Football, GGML waliamua kusaini makubaliano ya udhamini huo kwa sababu pia ni sehemu ya jamii ya Geita.

Zahara Michuzi alifichua kuwa Geita ina vipaji vingi na wanasoka wazuri, sababu zilizoifanya serikali kuwa na nia ya kuibua uwezo wao kwa kuhamasisha wawekezaji zaidi kuwekeza katika mchezo wa soka.

“GGML ni moja ya mwekezaji mzuri ambaye amekuwa akitekeleza miradi kadhaa endelevu. Uwekezaji wa GGML mkoani Geita umekuwa wa kushangaza,” alisema.

Akitoa maoni yake kuhusu hatua hiyo, Mwenyekiti wa Klabu ya Geita, Leonard Bugomola alipongeza GGML kwa udhamini huo huku akiahidi kujitolea na kuhakikisha wachezaji wanakuwa na matarajio ya kufika kileleni mwa Ligi Kuu.

Tangu kuanzishwa kwake, GGML imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na mamlaka za serikali za mitaa kusaidia miradi kadhaa ya jamii katika mkoa wa Geita kupitia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na programu za kitaifa.


## MECHI ZA USHINDI

“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE “2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 27 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3488 | Barwell vs Coalville Town | 3.51 | 4.04 | 1.76 |
| 15:20 | 5812 | Al Raed Club vs Al Ahli Jeddah | 2.44 | 3.41 | 2.72 |
| 15:30 | 3984 | Doncaster vs Sunderland | 5.28 | 3.81 | 1.59 |
| 16:00 | 3982 | St Ives Town vs Biggleswade Town | 2.55 | 4.04 | 2.17 |
| 16:00 | 5090 | Banbury United vs Stratford Town | 1.40 | 4.65 | 5.81 |
| 16:00 | 5260 | Royston Town vs Hitchin Town | 1.58 | 4.14 | 4.43 |
| 17:00 | 4511 | Northeast United FC vs Mumbai City FC | 3.81 | 3.52 | 1.81 |
| 17:50 | 5947 | Al Shabab Riyadh vs Al Taawon | 1.78 | 3.82 | 4.07 |
| 18:00 | 1120 | Kings Langley vs Chesham Utd | 3.30 | 3.80 | 2.03 |
| 18:00 | 1214 | Cliftonville Belfast vs Crusaders Belfast | 2.60 | 3.23 | 2.46 |
| 18:00 | 1708 | Bamber Bridge vs Lancaster City | 1.78 | 3.71 | 3.71 |
| 18:00 | 1987 | Whitby Town vs South Shields | 2.54 | 3.36 | 2.45 |
| 18:00 | 2349 | Redditch United vs Alvechurch | 3.27 | 3.61 | 1.93 |
| 18:00 | 2437 | Lowestoft Town vs Leiston | 2.56 | 3.96 | 2.19 |
| 18:00 | 2453 | Dorchester Town vs Poole Town | 2.70 | 3.57 | 2.23 |
| 18:00 | 2659 | Utd of Manchester vs Ashton Utd | 1.81 | 3.56 | 3.75 |
| 18:00 | 2890 | Atherton Collieries vs Radcliffe Borough | 2.06 | 3.46 | 3.08 |
| 18:00 | 3025 | Stafford Rangers vs Nantwich Town | 1.94 | 3.47 | 3.38 |
| 18:00 | 3132 | Tiverton Town vs Weston Super Mare | 2.66 | 3.58 | 2.25 |
| 18:00 | 3171 | Metropolitan Police vs Walton Casuals | 1.66 | 3.85 | 4.23 |
| 18:00 | 3226 | Hednesford Town vs Rushall Olympic | 2.61 | 3.72 | 2.23 |
| 18:00 | 3305 | Warrenpoint vs Dungannon Swifts | 2.51 | 3.38 | 2.46 |
| 18:00 | 3578 | Carrick Rangers vs Larne | 6.16 | 4.52 | 1.40 |
| 18:00 | 3595 | Mickleover Sports vs Basford United | 2.56 | 3.39 | 2.41 |
| 18:00 | 3620 | Matlock Town vs Buxton FC | 2.46 | 3.48 | 2.46 |
| 18:00 | 3651 | Linfield Belfast vs Glentoran Belfast | 1.99 | 3.42 | 3.28 |
| 18:00 | 3705 | Scarborough Athletic vs Morpeth Town | 2.08 | 3.52 | 2.99 |
| 18:00 | 3716 | Portadown FC vs Glenavon | 3.62 | 3.82 | 1.78 |
| 18:00 | 3788 | Ballymena Utd vs Coleraine FC | 3.57 | 3.47 | 1.88 |
| 18:00 | 4992 | Gosport Borough vs Hartley Wintney | 1.47 | 4.25 | 5.42 |
| 18:00 | 5088 | Derby vs West Bromwich | 4.32 | 3.43 | 1.80 |
| 18:00 | 5320 | Witton Albion vs Warrington Town | 2.97 | 3.50 | 2.09 |
| 18:00 | 5398 | Peterborough Sports vs Rushden and Diamonds | 1.59 | 4.34 | 4.15 |
| 18:00 | 5515 | Grantham Town vs Gainsborough | 2.90 | 3.47 | 2.14 |
| 18:00 | 5560 | Truro City vs Taunton Town | 2.41 | 3.61 | 2.45 |
| 18:00 | 5680 | Bromsgrove Rovers vs Stourbridge | 2.24 | 3.71 | 2.60 |
| 18:00 | 5744 | Stalybridge vs Hyde United FC | 2.22 | 3.43 | 2.80 |
| 18:00 | 5796 | Wimborne Town vs Salisbury City | 3.18 | 3.76 | 1.93 |
| 18:00 | 5959 | Nuneaton vs Tamworth | 2.70 | 3.85 | 2.13 |
| 20:00 | 2631 | Konyaspor vs Besiktas | 2.76 | 3.25 | 2.47 |
| 20:00 | 5387 | Kayserispor vs Sivasspor | 2.96 | 3.25 | 2.33 |
| 20:30 | 4325 | QPR vs Bournemouth | 2.80 | 3.29 | 2.39 |
| 20:45 | 3209 | Mechelen vs RFC Seraing | 1.65 | 4.03 | 4.52 |
| 20:45 | 4114 | Charleroi vs OH Leuven | 1.68 | 3.93 | 4.42 |
| 21:30 | 1767 | Maccabi Petach Tikva vs Maccabi Tel Aviv | 5.78 | 3.95 | 1.48 |
| 22:30 | 3112 | FAR Rabat vs Raja Casablanca | 2.77 | 2.86 | 2.57 |
| 23:00 | 2771 | St Truiden vs Eupen | 2.28 | 3.41 | 2.92 |
| 23:00 | 4477 | Kfco Wilrijk vs Anderlecht | 4.95 | 3.96 | 1.61 |
| 23:00 | 4788 | Newcastle vs Manchester Utd | 5.66 | 4.34 | 1.53 |
| 23:15 | 4541 | CF Estrela vs GD Chaves | 2.44 | 3.22 | 2.74 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo




Jumatatu Desemba 27, 2021
Nipashe

Saka ajifunga tena Arsenal UKURASA 21

# Pablo atoa hesabu 3 za Azam Simba

## ●●● Akitaka kikosi kuingia kambini leo tayari kujiwinda na mechi hiyo ya Jumamosi...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, tayari amegeuzia hesabu zake katika kuzisaka pointi tatu kutoka kwa Azam FC kuelekea mechi ya Ligi Kuu Bara wakati miamba hiyo itakapokutana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, alisema baada ya kutoka Tabora wamerejea na wachezaji kupewa mapumziko ya siku mbili kabla ya leo, Jumatatu wote kuingia kambini kwa muda waliopangiwa.**

Alisema lengo ni kuanza mapema maandalizi ya mchezo huo wa Jumamosi kwa kila mmoja kufuata programu ya mazoezi na kuongeza utimamu wa mwili.



"Kocha Mkuu (Pablo), amesisitiza wachezaji kuwahi kwa kuzingatia muda wa kurejea kambini ili kuanza pamoja programu ya mazoezi.

"Hataki mchezaji yeyote kubaki nyuma, wachezaji wote wanatakiwa kuwa sawa kwa utimamu wa mwili na kuhakikisha kila mmoja anakuwa tayari kwa majukumu ambayo atapewa kuelekea mechi yetu dhidi ya Azam FC," alisema Hitimana.

Alisema anatarajia mchezo huo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja wao anahitaji matokeo chanya, lakini wao wanazihitaji zaidi pointi tatu kuelekea kutimiza malengo yao ya kutetea ubingwa.

Hitimana alisema malengo yao ni kuhakikisha wanapata alama tatu katika kila mechi ya ligi ili kujihakikishia kutetea ubingwa wao kwa mara nyingi kwa msimu huu.

"Ligi imekuwa ngumu na ushindani ni mkubwa, kila mmoja anahitaji kupata matokeo chanya, hivyo Pablo amewasisitizia wachezaji kutochelewa kurejea kambini kwa ajili ya kuendelea pale tulipoishia kuelekea mchezo wetu dhidi ya Azam FC," alisema Hitimana ambaye kwa pamoja na Selemani Matola ni wasaidizi wa Pablo.

Simba ambayo ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 21, mbili nyuma ya Yanga kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya Biashara United, itakuwa mwenyeji wa mchezo huo utakapogigwa Uwanja wa Mkapa.

Azam FC, ambayo imeshashuka dimbani mara 10 msimu huu bado haijaonyesha makali yake kwenye mbio za ubingwa kwani ipo katika nafasi ya saba ikiwa na pointi 15.

Baada ya mechi hiyo, Simba, Yanga, Azam na Namungo zitaelekea Zanzibar tayari kwa michuano ya Mapinduzi Cup inayotarajiwa kuanza Jumapili wiki hii Namungo kukata utepe dhidi ya Meli 4 City.

Simba ipo Kundi C pamoja na Selem View na Mlandege FC, wakati Kundi B, linaundwa na Yanga, Taifa Jang'ombe na KMKM SC huku Kundi A likiwa na Azam FC, Namungo, Yosso Boys na Meli 4 City.

'OOOH YES'...




Kipa wa Yanga, Djigui Diarra, akiwa mazoezini. Jana usiku waliikaribisha Biashara United kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: MAKTABA**

# Sure Boy apeperusha nyota wa kigeni Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema kuwa imemsajili mchezaji Salum Aboubakar 'Sure Boy' kutokana na uwezo wake uwanjani na si mapenzi yake kwa klabu hiyo kama wengine wanavyodhani.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, alisema mchezaji huyo ambaye alitambulishwa juzi klabuni hapo, baada ya kushindwana na klabu yake ya Azam na kuamua kuachana kwa amani, alihitajika Yanga tangu msimu uliopita, lakini ilishindikana.

Akizungumzia usajili wa mchezaji huyo, alisema kuwa hakuwa kwenye malengo kwa kipindi hiki cha usajili kama wengi wanavyodhani, lakini baada ya kuachana na klabu yake na kumruhusu kuondoka ndipo na wao wakaanza utaratibu kama wanaweza kumsajili, na bahati nzuri wakafanikiwa.

"Yanga haisajili mchezaji kwa mapenzi, ila uwezo wake sisi tulihitaji kiungo mchezeshaji ili kama Khalid Aucho hayupo, basi huyu anacheza. Kocha anahitaji kuwa na machaguo mengi, akitoa moto anaingiza moto, siyo akitoa moto anaingiza maji ya vuguvugu," alisema Bumbuli.

Akisimulia jinsi kiungo huyo alivyosajiliwa, alisema ilikuwa ni kama bahati kwani tayari walikuwa wanafanya mazungumzo na mchezaji mmoja nje ya nchi.

"Tulikuwa tunafanya mazungumzo na mchezaji mmoja nje ya nchi kiungo mchezeshaji, mara tunasikia jamaa ameachana na timu yake, usiku huo huo tukapigiana simu viongozi tukaambizana kama kuna uwezekano wa kuonana na meneja wake, Heri Mzozo, yaani mpaka asubuhi tu inafika kila kitu tayari, ilikuwa kama kuokota dodo chini ya mwarobaini," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >